

UWEKEZAJI

 Habari za asubuhi, kwa kila mmoja. Nina furaha sana kuwa hapa. Mimi kidogo ni mfupi. Huna budi kukivuta *hiki* chini kidogo. Kidogo hili ni jambo ambalo sikulitarajia, kuwa hapa asubuhi ya leo, kwa sababu nilipaswa kuondoka mjini asubuhi ya leo saa thenashara, kwenda kama maili mia moja na hamsini kaskazini mwa hapa, pamoja na marafiki fulani. Na kwa hiyo waliponiambia nilipaswa kuwa hapa asubuhi ya leo kuzungumza kwenye kiamshakinywa, kidogo ilinibidi kuharakisha na kubadilisha ratiba yetu kidogo. Daima ni majaliwa, hata hivyo, kuwa mahali watu wa Bwana walipo. “Ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai.”

² Nami nina furaha sana kuwa hapa na kukutana na marafiki zetu wote tena, ushirika huu mzuri. Mnaweza kuwazia jinsi ninavyojisikia, nikisimama hapa pamoja na mtu ambaye amekuwa akihubiri Injili nilipokuwa jamaa mdogo sana, na—na hiyo ni kuchukua muda mrefu sana huko nyuma. Basi, lakini, nina shukrani sana kukusanyika hapa pamoja na watu.

³ Na sasa, usiku wa leo ni usiku mwingine mkuu, tunamtarajia Mungu kufanya mambo makuu.

⁴ Basi kote katika juma hili, nimekuwa na majaliwa ya—ya kwenda huku na huku kupitia Bonde la Maricopa hapa, nikizungumza na watu katika makanisa yao. Nasi tumekuwa na wakati mzuri. Ninashukuru sana kwa ajili ya ninii yake... ushirika, na wa Roho Mtakatifu miongoni mwa watu Wake.

⁵ Basi ninaitazamia, pia, Jumapili jioni, wakati mimi...ni majaliwa yangu kuzungumza tena Jumapili alasiri. Na, halafu, Jumatatu usiku kwenye dhifa. Sasa, ninatumainia ya kwamba yote yanayofanywa ama kusemwa, tuta—tatakuwa na upeo mkubwa Jumatatu usiku. Ndugu Oral Roberts amechaguliwa kuzungumza kwenye mkutano huu wa dhifa. Na sisi ni... Tunataka kumwombea. Ombeni ya kwamba Mungu atampa ujumbe ambao uta—utaipeleka Phoenix magotini mwao, wakitetemeka, mnaona, kuutikisa Uwepo wenyewe wa Mungu mbe—mbele ya watu. Nasi tunatumaini ya kwamba hilo litatimia.

⁶ Na kote kwenye huo mfululizo, kila kitu kinachofanywa, tunatumaini itaacha ushawishi mwingi sana Phoenix, hata kamwe hawawezi kuwa vile vile. Nao watu ambao wamekuwa hapa na watarudi katika miji yao wenyewe, hawatarudi jinsi walivyotoka. Watarudi, wamevuviwa, na wakiwa na azimio zaidi kufanya kazi ya Bwana, pamoja na ono jipya kutoka kwa Mungu.

⁷ Nipo hapa kwa sababu ya ono. Na kama yeyote wenu amewahi kuchukua yoyote ya kanda...mimi si mwuza kanda.

Bila shaka, tuna shughuli ya kanda kote ulimwenguni. Lakini kama umewahi kununua kanda kutoka kwangu, ama, sio kutoka kwangu, bali kutoka kwa Bw. Maguire. Yeye yupo hapa mahali fulani, akinasa kanda, asubuhi ya leo, nadhani. Chukua hiyo, *Ni Wakati Gani, Bwana?* Nimesimama mahali hata si—sijui hatua ya pili.

⁸ Nimeona maono tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Jambo la kwanza ninaloweza kukumbuka, karibu la kwanza, maishani, lilikuwa ni ono. Na mimi, mbele ya watu kutoka mahali popote, ninamwomba mtu yeyote kuniambia wakati mmoja ambapo moja ya hayo liliwahi kushindwa. Haliwezi kushindwa. Ni Mungu.

⁹ Kwa hiyo, hili limeniweka katika hali kwamba ni—nikianza kuliwazia, nalo linanifarakanisha tu kabisa. Nami najua jambo fulani litatukia. Na mimi—mimi ningeogopa . . .

¹⁰ Ni kama tu vile nilivyokuwa nikimwambia mtu fulani hivi majuzi. Tunatambua ya kwamba hatutaki kumchukua Mungu na kulifanya liwe tu vitimbi sasa. Wala hatutaki kuchukua karama za Mungu na kufanya vitimbi kutokana nazo. Unaposema Bwana alisema jambo fulani, kuwa na hakika Bwana alikwambia; isiwe ni dhana. Unaona? Kuna mengi sana ya hayo sasa, mnaona, nao watu hawajui jinsi ya kuwa na matumaini. Mungu akisema lolote, halina budi kuwa ni hivyo hasa. Sharti litukie jinsi hiyo.

¹¹ Hivyo ndivyo tunavyoweza kuiamini Biblia. Hapo mwanzo, iliahidi Masihi. Hao manabii wa Kiebrania walinena juu ya Masihi, yale Yeye angefanya. Huyu Masihi alikuja vile hasa ilivyokuwa. Biblia, kwa upande mmoja, inasema itatukia wakati fulani. Inatukia, moja kwa moja.

¹² Sasa, tuna matumaini ya kwamba kutakuwako na Unyakuo. Yesu atakuja. Tuko papa hapa. Kwa sababu, haliwashindwa kamwe mahali pengine popote, wala haliwezi kushindwa sasa. Hayo ndiyo matumaini yetu.

¹³ Kama wakati, Yeremia, Bwana alikuwa amemwambia, aweke nira hiyo shingoni mwake. Haijalishi ni nabii yupi au nini kingine kilisema hilo, kitu chochote kinyume na hiyo miaka sabini huko chini Babeli, itabidi iwe hivyo. Hata hivyo, Hanania aliinuka, nabii, na mwana wa nabii. Ndipo akaichukua nira hiyo kutoka shingoni mwa Yeremia, akaivunja, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, katika miaka miwili watarudi.”

¹⁴ Kasema, hata nabii Yeremia alisema, “Amina, Hanania, Bwana na ayatimize maneno yako. Lakini hebu tukumbuke, kumekuwako na manabii waliotutangulia. Na wakati . . . Nabii anajulikana tu wakati unabii wake unapotimia.”

¹⁵ Nafikiri hilo ni somo zuri sana la Kipentekoste. Mnaona? Tunaweza kushawishiwa, kuchochewa, na tunaweza kuwa na furaha na baraka za Bwana. Lakini tunaponena katika Jina la

Bwana, na kama tunayonena hayalingani kabisa na Neno hilo, kaa mbali nayo. Sijali linaonekana la kupendeza jinsi gani.

¹⁶ Kwa kuwa, *Huu* ndio ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Dumu na Neno hilo. Usiliache Hilo, kwa chochote kile. Unaona?

¹⁷ Sasa, mnaona, laiti Hanania angaliwazia tu, ufunuo huo. Wala siamini mtu huyo alikuwa ni mnafiki. Alikuwa amevuviwa. Ila haukulingana na Neno. Hauna budi kuwa ni Neno.

¹⁸ Basi wakati mmoja ilitukia tena, hapo wakati Yehoshafati aliposhuka kumtembelea Ahabu. Nao wakafanya baraza, na kukwea kwenda Ramoth-Gileadi. Naye Yehoshafati akasema, “Vema, hakika, magari yangu ni kama magari yako, watu wangu ni kama wako.” Akasema, “Lakini hivi hatupaswi kumwuliza Bwana?”

Ahabu akasema, “Hakika inatupasa kufanya hivyo.”

¹⁹ Kwa hiyo walikuwa na manabii mia nne wa Kiebrania; sio manabii wa Baalimu, sio makafiri, bali manabii wa Kiebrania. Zedekia akajitokeza na pembe mbili kubwa, akasema, “BWANA ASEMA HIVI. Kwa hizi utawasukuma Washami kabisa watoke nje ya nchi.” Kimsingi, alikuwa sahihi, bali kuna mengi zaidi yanayoambatana nayo mbali na hayo.

²⁰ Unaweza ukawa sahihi kabisa kimsingi, hata hivyo ahadi za Mungu zimewekwa msingi juu ya masharti.

²¹ Walikuwa wakiweka dhabihu zao kwa kicho tu walivyoweza, wakifanya yale Bwana aliyowaambia, hata hivyo pasipo na unyoofu nyuma yake. Matoleo, ikawa ni desturi ya familia.

²² Huko ndiko tunakoipeleka Pentekoste: desturi ya familia. Inatupasa tuwe waaminifu zaidi ya hivyo. Mkimtarajia Mungu kujibu baraka hizi na ahadi, rudini kwenye unyoofu wa Neno hilo. Yale Neno lisemayo, dumuni na Hayo.

²³ Sasa, nabii huyu kimsingi alikuwa sahihi. Mungu alipoigawa hiyo nchi, kwamba Yoshua aliwapa Israeli hiyo. Na hawa hapa adui, walikuwa wakijaza matumbo yao kwa ngano iliyolimwa Ramothi. Na kimsingi ni kweli, ila, mnaona, ilikuwa ni kwa masharti. Nao hao manabii, ama wahudumu, wakitabiri, walikuwa sahihi kabisa. Kisha walisema . . .

²⁴ Kwa mtu huyu wa Mungu, Yehoshafati, ilionekana kuna kitu kinyume kidogo. Akasema, “Hivi hakuna mwingine mmoja?” Ati mwingine mmoja, baada ya kuwa na mia nne? Mbona, ilionekana ni dhihaka. Lakini, hata hivyo, ndani kabisa kwenye kilindi cha moyo wa mtu huyo yeye alijua kuna kasoro fulani.

²⁵ Mtu yeyote wa Mungu anaweza kuona kuna kasoro fulani. Baraka zetu ni sawa, bali hazifikii kwenye kile kiwango.

²⁶ Kwa hiyo akaona kulikuwa na kasoro fulani. Kasema, “Hivi hakuna mmoja zaidi?”

27 Kasema, “Naam, kuna mmoja zaidi. Mikaya, mwana wa Imla. Lakini,” kasema, “Ninamchukia.” Kasema, “Yeye daima anaturarua-rarua na kutukemea.”

Akasema, “Mfalme na asiseme hivyo. Bali hebu tumsikilize.”

28 Na kwa hiyo wakaagizia aje. Nao wakasema, “Sasa, umefukuzwa kwenye shirika, muda mrefu vya kutosha. Sasa, unaweza kuja huku na useme jambo fulani sawa na wanavyosema, na litakuwa sawa.”

29 Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale Yeye anayoweka moyoni mwangu,” ndivyo alivyowaambia. Tunahitaji Imla tena. . . Tunahitaji Mikaya, hasa.

30 Ndipo yeye, usiku huo, akaomba amngojee Bwana. Ndipo alipoona ono la Bwana, basi akalichunguza hilo na Neno. Na alipolichunguza na Neno, Neno na hilo ono yalikuwa sawa. Ndipo akasimama mbele zao na kuwaambia yale yangetukia.

31 Basi, bila shaka, mnajua Zedekia alimchapa kofi kinywani, na kusema, “Neno lilienda wapi, Bwana alienda wapi hapo aliponiacha? Roho wa Bwana, wakati aliponiacha?”

Akasema, “Utaona.”

32 Ahabu akasema, “Mtieni jamaa huyu katika gereza la ndani. Mpeni chakula cha shida.” Kisha kasema, “Basi nitakaporudi, nitamshughulikia.”

Akasema, “Ukirudi kamwe, Bwana hajasema nami.”

33 Mnaona, halina budi kuafikiana na Neno, nasi hatuna budi kukumbuka hilo. Hata hivyo, si—sikuja kusema hilo.

Hebu tuombe. Na tuviinamishe vichwa vyetu, kila mmoja.

34 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja asubuhi ya leo katika Jina la Bwana Yesu. Na hapa Wewe umenipa asubuhi ya leo, Bwana, kundi hili zuri la watu, ili niweze kuzungumza maneno machache kwa wafanyabiashara hawa kutoka kote nchini. Bwana, naomba ya kwamba Wewe utatujalia hili asubuhi ya leo kwamba kutakuwa na jambo litakalosemwa ambalo halitakuwa ni mtu tu akisimama hapa kuchukua muda fulani ama kutumbuiza, lakini Neno la Bwana lipate, kwa njia isiyojulikana, hata kwetu sisi, kutolewa, ambalo lingefanya jambo fulani kuwasaidia watu, saa hii kuu. Waponye wagonjwa, wanaoteseka.

35 Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utaichochea mioyo ya wafanyabiashara hawa. Wabariki wahudumu, waaminio Wako wa awamu zote mbalimbali, na sehemu, na karama, na maofisi ambako Wewe umewaweka. Pia jalia twende asubuhi ya leo pamoja na—na msimamo ule ule wa wale waliotoka Emau, wakisema, “Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?” Jalia Roho Mtakatifu aje sasa na kusema na mioyo yetu kwa dakika chache

zijazo, kupitia kwa Neno. Tujalie hilo, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

³⁶ Sasa kwenu ninyi mnaopenda tu kuchukua muhtasari kidogo, nimeandika hapa chini, kidogo kunikumbusha. Nilikusudia kwenda mahali fulani leo hii, bali sikuzote ni Neno la Bwana, ama nafasi za kuzungumza kwa ajili Yake, hutangulia. Hatujui ni wakati gani tutakapouacha ulimwengu huu, nasi tunataka kutia kila chembe ya wakati tujuavyo.

³⁷ Ninataka kusoma asubuhi ya leo kutoka Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 19, kuanzia kifungu cha 16, kwa somo dogo tu, kutoa kutoka hapa, iwapo Roho Mtakatifu anapenda, muktadha.

Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu Mwema, nitende jambo gani jema, ili nipate kuurithi uzima wa milele, ama nipate uzima wa milele.

³⁸ Ninataka kusimama kwa dakika moja.

. . . ni jambo gani jema ningeweza kutenda, nipate uzima wa milele?

Akamwambia, Mbona unaniita mimi mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri.

Yeye akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo,

Waheshimu baba yako na mama yako, . . . Mpende jirani yako kama nafsi yako.

Yule kijana akamwambia, Haya yote nimeyashika tangu utotoni . . . nimepungukiwa na nini tena?

Yesu akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo . . . unifuata.

Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni.

. . . tena nawaambia, Ni rahisi zaidi ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika . . . ufalme wa Mungu.

Nao wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, Ni nani basi awezaye kuokoka?

. . . Yesu—Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.

³⁹ Sasa ningetaka kutoa, kutoka kwenye kitu hiki kidogo hapa, muktadha, ikiwezekana, mkiniruhusu, dakika chache tu. Sasa, tunaweza kuliwazia tukio hilo.

⁴⁰ Na kwa kuwa hiki ni kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, Jumamosi asubuhi ni kiamshakinywa cha kawaida, ninaamini. Nilikuwa na majaliwa ya kuzungumza Jumamosi iliyopita asubuhi.

⁴¹ Ambalo, ninathamini mwaliko huu kutoka kwa ndugu hawa wazuri ambao huniruhusu mimi kuja, katika uhaba wangu wa elimu, na mbele ya watu werevu na walioelimika, na kujaribu kuuleta Ujumbe huu ambao ni—ninajisikia ya kwamba mioyo yetu inahitaji. Na mimi—mimi nathamini hilo, wakati milango mingi inafungwa upesi nyuma. Kwa hiyo ni—ninashukuru kwa ajili ya watu hawa, na bila shaka ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki.

⁴² Jumamosi iliyopita asubuhi, nilijaribu kuleta Ujumbe ambao ungekuwa ndio niliowazia ungehitajika. Nilizungumza juu ya Uzia, jinsi ambavyo alikuwa ni mtu mashuhuri, mfano mbele ya Isaya. Lakini wakati alipoingiwa na kiburi, basi akajaribu kupachukua mahali pa—pa kuhani, mhudumu. Na, katika kufanya hivyo, Mungu alimpiga kwa ukoma. Basi lilikuwa ni somo kubwa kwa Isaya, kujua kutotumainia (kitu) chochote ila Mungu. Basi alikuwa hekaluni, akaona ma—mahali.

⁴³ Niliwasihi ndugu zangu. Msijaribu kuchukua mahali pa chochote ila mfanyabiashara, chochote Mungu amekuwa kufanya. Msijaribu kuwa wahubiri, maana tuna wakati mgumu kutosha, kuliweka Hilo limenyoka, kwa vyovyote vile. Nawe unalichanganya Hilo. Kwa hiyo hebu tukae tu jinsi Mungu anavyotuita tuwe. Nami nawazia, kwa walei, ni jambo zuri kwetu kujaribu kubaki.

⁴⁴ Usijaribu kumwiga mtu mwingine. Unaona? Kuwa tu kile ulicho. Sote tungetaka kuwa Billy Graham, Oral Roberts. Sote tungetaka kuwa hivyo. Lakini, kumbukeni, katika ufalme wa Mungu na uchumi Wake mkuu, kama tutakuwa jamvi la mlangoni, kama hapo ndipo mahali petu, tutakuwa tu kadiri walivyo wao. Mnaona? Lakini huna budi kudumisha mahali pako ambapo Kristo amekuweka.

Ningetaka kuzungumza asubuhi ya leo sasa juu ya: *Uwekezaji*.

⁴⁵ Sasa, karibu kila mfanyabiashara mzuri anavutiwa na uwekezaji mzuri. Nilichagua hili kwa sababu ilikuwa ni wafanyabiashara, ambao wangevutiwa na uwekezaji. Na karibu watu wote wanapenda hilo, uwekezaji, na hasa sana inapaswa kuwa ni jambo zuri sana kwa kundi la wafanyabiashara. Nasi daima tunajaribu kupata mahali fulani kufanya uwekezaji kidogo, kupata dola chache, ama, na hilo ni sawa. Sina la kusema dhidi ya hilo. Hilo ni sawa kabisa.

46 Lakini ninawazungumzieni juu ya uwekezaji mzuri kuliko wote nijua, kufanya uwekezaji; mahali pazuri zaidi, hasa, kuwekeza.

47 Biashara nzuri, ama mfanyabiashara mzuri, anajua vema kuliko kucheza kamari. Usicheze kamari; utapata hasara. Huwezi kushinda, kucheza kamari. Wewe ni fukara wakati mmoja, tajiri wakati huo mwingine, kisha unarudi kuwa fukara tena. Kucheza kamari ni ugonjwa. Ni pepo mchafu tu. Naye huja juu ya watu, wakati mwingine, katika namna ya polepole. Unaweza kucheza kamari katika dini. Huenda usijue hilo, bali unaweza.

48 Ni kama tu kama taifa lingeacha kuona... Mnamwacha mlevi atoke hapa nje mtaani akiwa na—akiwa na—akiwa na gari lake. Mtu huyo anapaswa kupata kifungo cha angalau miaka kumi gerezani. Mnamwacha mtu kushuka mtaani, asubuhi ya leo, akiwa na—akiwa na bastola mkononi mwake, akifyatua risasi kote namna hiyo, wangezitupilia mbali funguo za mtu huyo. Wangemfunga katika gereza la ndani. Halafu mlevi anaweza kushuka mtaani, yeye kabisa yuko kwenye hatari ya kumwua mtu kama mtu aliye na bastola, naye anatozwa dola tano kwa ajili yake, ama kitu fulani. Mnaona? Mnaona? Yeye, yeye ni... Karibu ni mauaji ya kudhamiria. Lakini, mnaona, taifa haliliangalii namna hiyo.

49 Wala na watu, wakati mwingine, wakati wanapocheza kamari, kidogo, hali ya polepole, ya kusema, “Loo, vema, mimi—mimi ni mzuri kama hao wengine.” Huko ni kubahatisha. Usifanye hivyo. Hiyo ni biashara mbaya.

50 Mfanyabiashara yeyote mzuri hapaswi kuchukua pesa zake na kucheza kamari. Na—na baadhi... Waaminio hawapaswi kucheza kamari kamwe. “Loo, vema, hii ni sawa. Nitabahatisha kwa hii.” Usifanye hivyo.

51 Kuna kielelezo kilichowekwa, kitu halisi, na Hicho si cha kundi lolote lile la watu. Ni Neno la Mungu. Usibahatishe kwa Hilo. Sasa, usibahatishe.

52 Pia jambo lingine nilionalo miongoni mwa watu, wakati mwingine, hususan. Mtu anapata pesa kidogo, halafu atajaribu kuiwekeza katika namna fulani ya lala maskini-amka tajiri, biashara isiyotambulikana. Utapoteza shati kutoka mgongoni mwako, nawe unajua hilo. Unaona? Usijaribu hilo. Naye mfanyabiashara mzuri, mwenye akili timamu hatafanya hivyo. Mtu asiye na uzoefu wa kazi ndiye atakayebahatisha hivyo. Kamwe haina faida.

53 Loo, ni visa vingapi ambavyo nimeona wakati wangu, ambapo watu walikuwa na akiba ya maisha yao, nao wanatoa kifaa kidogo, kutajirika upesi, upesi sana, na yote namna *hii*. Nao wakaipata. Halafu, muda si muda mwajua, wanajikuta

kwenye—kwenye mtelezo, mahali fulani, wakijaribu kuridhisha ninii yao . . . ama kupoteza mawazo yao kwa yale wamefanya.

⁵⁴ Na hilo lingetumika pia katika anga za Ukristo. Baadhi ya utajiri wa ghafla, kupeana mikono na mhubiri, na kuliandika jina lako kwenye kitabu, na yote yamekwisha. Kamwe usiamini upuuzi kama huo. Haifanyi kazi. Haina budi kutokea kwa njia moja.

⁵⁵ Huu utajiri wa ghafla, haufai. Mfanyabiashara mzuri hatajipumbaza nao. Kama una chochote, chochote unachotaka kuwekezea, tafuta biashara iliyotambulishwa, kitu ambacho kimethibitishwa. I—inatimiza . . . Inatimiza ahadi yake. Ina faida.

⁵⁶ Na hili hapa jambo lingine. Usiweke fedha zako mfukoni mwako. Kamwe hutapata chochote. Mtu fulani atakuibia hizo, baada ya kitambo kidogo. Naam. Mnaona? Hutaki kufanya hivyo. Yesu alifundisha jambo lilo hilo. Ukiwa na talanta, usi—usiifiche. Inakupasa kuitumia, ikue.

⁵⁷ Sasa, huenda ninazungumza na Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti, kwenye viamshakinywa hivi, na kadhalika. Kamwe hujui ni nani anayeketi mbele yako. Unaona?

⁵⁸ Kwa hiyo, kumbuka, kama una kitega uchumi, kitu fulani cha kuwekeza, wekeza katika kitu kizuri, kitu kilicho halisi, kitu ambacho kimethibitishwa ambacho kitaleta faida, kampuni nzuri, inayoweza kutegemewa, iliyotambulikana, iliyothibitika kuwa na faida, wakati uliopita. Inajulikana vizuri. Ninyi wanaume mnajua hilo.

⁵⁹ Hata kama itakubidi kuzipokea polepole, zikija, migawo yako—yako ni—ni midogo zaidi. Hata hivyo, ni heri nijue, pesa zangu zote, nilikuwa nikipata asilimia mbili, na nina hakika kuipata, kuliko kupata asilimia hamsini wala sizipati kamwe; kuahidiwa asilimia hamsini. Mnaona, unataka—unataka kukaa na shirika ama—ama biashara iliyo na msingi, ina sifa nyuma yake, kitu ambacho kitakuwa na faida, na kitu ambacho ni cha kweli.

⁶⁰ Sasa, jamaa huyu mdogo ambaye tunazungumza habari zake, kijana huyu mfanyabiashara, mbona, alikuwa—alipewa nafasi ya kuwekeza katika moja ya biashara kubwa sana angaliweza kuwekezea. Alipewa nafasi ya kumfuata Yesu Kristo. Na ni ja—jambo la dhihaka jinsi gani alilofanya. Ni jambo la kijinga jinsi gani, ambalo, jamaa huyu mdogo, akiwa amepewa nafasi ya namna hii, kuiwekeza na—nafsi yake na pesa zake, na chochote alichokuwa nacho, katika Ufalme wa Mungu, naye akaikataa, kabisa. Tunamwangalia asubuhi ya leo, kama kijana mfanyabiashara huyu, kama—kama mfanyabiashara duni sana. Ila usingalimwambia hilo. Yesu asingeweza kumwambia vizuri zaidi.

⁶¹ Mnaona, Neno la Mungu, Yesu anaponena, Hilo ni—Hilo lote ni Kweli. Halihitaji kufafanuliwa. Mungu huzungumza tu Kweli, wala haimbidi kuzunguka kama tufanyavyo, kujaribu kulielezea. Hilo, Ndilo Hilo. Hayo ndiyo yote kulihusu. Yeye alisema, “Unifuata.” Hivyo tu. Haikumbidi kumwambia ni kwa nini, kulielezea Hilo kama nifanyavyo mimi, na watu wengine wafanyavyo. Bali Maneno Yake yote ni Kweli. Haitubidi kuzunguka Nalo. Liseme tu. Yeye alisema, “Unifuata,” na hilo latosha.

⁶² Alikuwa na mwaliko kuwekeza katika Yesu Kristo. Basi huyo ndiye Mtu ninayezungumza habari zake asubuhi ya leo, uwekezaji ninaotaka mfanye, kama hamjaufanya.

⁶³ Lakini huyo jamaa mdogo tajiri, tineja wa siku zake, labda alikuwa na mrithi, pesa nyingi. Na—na, ambalo, hilo ni sawa. Hakuna neno dhidi ya hilo. Na mimi nita—mimi nitashukuru kwa ajili ya mwanamume yeyote ama mtu yeyote ambaye amepewa majaliwa hayo. Lakini wakati ninii... Kile nilicho nacho dhidi ya jamaa huyu ni hiki: akiwa ni mtu wa biashara...

⁶⁴ Basi mliona, yeye aliomba Uzima wa Milele? Hilo lilikuwa ndilo suala lake la biashara, “Nifanye nini sasa nipate Uzima wa Milele?” Naye Yesu akamwambia vile hasa alivyopaswa kufanya. Lakini haikumvutia, kwa sababu ya jambo alilopaswa kufanya, ku—kuupata Uzima wa Milele.

⁶⁵ Na sasa tunaangalia jambo hilo, sisi Wapentekoste, na kuwazia ya kwamba mtu huyo alikuwa amerukwa na akili zake, asifanye lolote. Lakini hebu—hebu tulilete nyumbani kwa dakika chache. Mnaona, kuna jambo fulani lililoambatana nalo.

⁶⁶ Aliulizwa juu ya amri. Akasema, “Hizo nimezishika tangu utotoni.”

⁶⁷ Labda alilelewa katika—katika nyumba nzuri, ya kiorthodoksi, ambamo walilelewa, wasiibe, wala kusema uongo, au kudanganya, wala kufanya uzinzi. Labda mvulana huyo hakuwa mdanganyifu. Mvulana huyo hakuwa ni mwongo. Alikuwa amelelewa na wazazi wazuri, mtu ambaye alikuwa amemfundisha kwamba kulikuwako na Mungu, na kwamba Mungu huyo atamleta hukumuni siku moja, naye itamlazimu kutoa hesabu kwa ajili ya yote aliyofanya. Basi mafundisho hayo ya—ya mzazi wake huenda yalikuwa yamebaki naye, naye alijua ya kwamba kulikuwako na—na Mungu.

⁶⁸ Lakini sasa inafikia wakati ambapo hana budi ku—kukutana na Mungu huyu binafsi. Hana budi kukutana na Mtu huyu. Basi akaulizwa ni nini... Aliuliza kile angeweza kufanya, na kuupata huu Uzima wa Milele, naye Yesu akamwambia la kufanya. Lakini hakuvutiwa na uwekezaji wa namna hiyo, kwa sababu uliondolea mbali mambo aliyokuwa ameyashikilia kwa kuyathamini sana.

⁶⁹ Vema, unasema, “Mtu huyo alikuwa na pesa, nao uliondolewa kwake kwa sababu ya pesa, hasa. Yesu alikuwa akiichukua kwa sababu kwamba hiyo ilikuwa ni mali yake ya duniani.”

⁷⁰ Lakini kwa jumla halimaanishi pesa. Kuna mambo mengi tu tunayoyashikilia kwetu sisi, kadiri tu ya sanamu, kadiri kijana mwanamume huyo alivyoshikilia pesa hizo; umaarufu, tofauti za kimadhehebu, mitindo, tamaa ya ulimwengu, sanamu, kila kitu. Yapo mambo mengi sana ambayo—ambayo watu, leo hii, badala ya kuwa tajiri, kushikilia mambo, wale wenye pesa, wao—wao wanashikilia mambo mbalimbali namna hiyo, kwa dhati tu kama kijana huyo mwanamume, kwa sababu hawavutiwi na uwekezaji ambao Kristo anawapa.

⁷¹ Huenda ikamaanisha ya kwamba Kristo angekuita kutoka kwenye kundi ulilomo. Huenda Kristo akakuita kutoka kwenye karamu ya kadi mliyo nayo kanisani mwenu, mchezo wa karata, chama ambacho wewe ni mshiriki. Unapolishikilia hilo, wewe ni—wewe unafanya kosa la kijinga tu kama kijana huyu mwanamume tajiri alivyofanya. Unaona? Unashikilia kitu fulani kana kwamba ni hazina kubwa kuliko kuwekeza safari yako ya maisha katika Yesu Kristo.

⁷² Sasa, hili huenda lisiwe na msingi wa kupigiwa makelele, bali lina msingi wa Injili kwake, wa Neno. Mnaona? Ndilo jambo ambalo... Watoto hucheka, na kucheza, na kushangilia, na kadhalika. Bali inakupasa kujua kwa nini unafanya hivi; la sivyo, hiyo inakuwa ni ibada ya sanamu kwako, unaona, inakuwa sanamu tu. Na kama tukiangalia, na kuona katika—katika hali tunayoingilia! Inaingia kwa kunyemelea sana.

⁷³ Ni kama tu mtu, mti, unaosimama kwenye ba—barabara kuu. Ndipo mzabibu mdogo unamea, mzabibu mwitu, na kuanza kujizungusha kwenye mti huo. Huo mti unataka kukua mnyofu, bali mzabibu huo hatimaye unaushika mti huo hivi kwamba unalazimishwa kupinda upande mwingine. Vivyo hivyo sisi huingia kwenye mahali pa namna hiyo, ambako tunaacha mambo mengine yapenyeze kwetu, na kutuzungusha kutoka kwenye uaminifu huo halisi katika Neno.

⁷⁴ Sasa, Israeli walikuwa waaminifu sana katika yale waliyofanya, hapo mwanzo. Loo, ninaweza kuwazia Myahudi akishuka barabarani, akiwa na dhabihu yake nzuri sana, nzuri sana aliyo nayo kwenye kundi lake, akishuka kwenda kwenye ka—kafara. Anaweka mkono wake juu ya huyo mnyama. Naye anajitambulisha na mnyama huyo, kwa kuuweka mkono wake juu ya mnyama huyu, halafu damu inamwagwa. Ndipo Myahudi huyo anarudi nyumbani, mwenye furaha tu alivyoweza kuwa, kwa sababu alijua alikuwa ametekeleza maagizo ya Yehova. Hiyo ilikuwa ni sawa kwa muda mrefu.

⁷⁵ Halafu, baada ya kitambo kidogo, jambo lilo hilo likawa ni desturi ya familia. Huyu hapo mnyama wa namna ile ile, bali mtu labda angesema, “Mwajua, huu ni mwezi mwandamo.” Labda, huenda ikawa, “Naam, sina budi kutoa dhabihu.” Wakati, Yeye alimpeleka kule chini jinsi yule mtu wa kwanza alivyofanya, lakini ha—hakuwa na unyofu huo kwake.

⁷⁶ Basi alipofanya hilo, Yehova alisema, “Kitu hicho kimekuwa uvundo puani Mwangu.”

⁷⁷ Ndipo akamwinua mtu mashuhuri jukwaani, nabii Isaya, ambaye alisema kwa sauti kuu, kasema, “Dhabihu zenu, sikukuu zenu zilizoamriwa, ni uvundo mbele Zangu.”

⁷⁸ Iweni waangalifu, Pentekoste. Dhabihu zenu na kushangilia zitakuwa uvundo katika pua za Yehova, endapo hazikuendewa kwa unyofu wa kilindi. Sisi, hatuna budi kuja kwa uaminifu kabisa, sio tu kucheka, na kushangilia, na kukusanyika kote. Hatuna budi kuja kwa kilindi na kwa uaminifu kwa Neno la ahadi. Hapo, tuyashike madhabahu, tukae hapo mpaka jambo fulani litukie, mpaka tumekufa kwelikweli, mpaka tuna—tunawezeza katika Ufalme wa Mungu na Yesu Kristo. Ndipo tuko kwenye. . . Haidhuru ni la kimsingi vipi. Tunaweza kuwa wa kimsingi, hata hivyo huna budi kuja chini ya uaminifu.

⁷⁹ Sasa, maskini Myahudi huyu alikuwa mwaminifu tu jinsi alivyoweza kuwa, katika yale aliyokuwa akifanya. Lakini wakati u—ulipowadia kuibadilisha kanuni yake ya imani, basi hapo ndipo shida ilipoingilia.

⁸⁰ Nashangaa kama Mungu yuyo huyo hana uwezo vivyo hivyo leo hii kutuiniua Isaya mwingine, kutuiniua mtu ambaye anaweza kutwambia ya kwamba sikukuu zetu za kuamuriwa zimekuwa uvundo. Inatupasa kuwa tayari kwa ajili ya Unyakuo, kwenye majira haya ya wakati. Angalieni mahali tulipo. Kuna kitu fulani kinachohitajika, na, hicho ni, kurudi kwenye Neno. Tumeahidiwa katika Malaki ya kwamba tutarudishwa kwenye Neno, Imani ya asili, na kwa hivyo hebu tukumbuke hilo sasa.

⁸¹ Lakini gha—gharama ambayo jamaa huyu mdogo alitakiwa kulipa ilikuwa ni kubwa mno. Ilimbidi kuuza mali yake yote ya ulimwengu, kusudi apate Uzima huu wa Milele.

⁸² Huenda usiwe na hela, bali hata hivyo unashikilia mambo, ambayo, ni mali ya ulimwengu.

⁸³ Kwa mfano, nimekuwa nikiwakemea wanawake wetu, sana, kuhusu kukata nywele zao na kuvaa nguo za kizinifu na kadhalika. Unawezaje kucheza katika Roho na kujiita Mpentekoste, na kuishi na roho kama hiyo juu yako? Ninyi wanaume mnawezaje kujiita watawala wa nyumba zenu, na kuruhusu kitu kama hicho? Ninawatakeni mfanye hesabu. Mnajua ni Kweli. Basi nyinyi hapo. Mnaona? Unaombwa kujitolea.

⁸⁴ Unasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Branham. Mimi ni raia wa Marekani. Mimi ni Mpentekoste. Mimi—mimi ni mfuasi wa Assemblies, ama ma—makundi hayo mengine, ama chochote kile. Nina haki ya Kimarekani kwa ajili ya hili. Na nikiwa ni Mkristo, ninayo haki, kwa sababu nimeikubali ile Dhabihu.” Hiyo ndiyo shida ya Marekani. Hapo ndipo lilipo katika tatizo, siku hizi.

Kila taifa linataka masihi fulani.

⁸⁵ Ndipo wakati Mungu alipowatumia Israeli Masihi, wote walikuwa wakiomba kwa ajili ya Masihi. Katika siku za kuja kwa Masihi, Israeli ilitaka jenerali ambaye angekuja na kuifukuza Rumi nje ya nchi kwa kishindo.

⁸⁶ Wakati uo huo, Rumi ilitaka masihi ambaye angekuja na—na kuwafanya mfumo mkuu wa utawala mpya wa kijeshi ambao unge—ungeiteka Misri na mataifa mengine yote, na kuwafukuza.

⁸⁷ Kila mmoja alitaka masihi. Na leo hii tunaona ni jambo lile lile. Ulaya...

⁸⁸ Vema, kwa mfano, Urusi, wanataka masihi ambaye anaweza kuwapeleka mwezini kabla ya mtu mwingine yeyote kufika kule.

⁸⁹ India inataka masihi, nao wanataka yule atakayewalisha pasipo kufanya kazi.

⁹⁰ Marekani inataka ninii... Wanataka mwenye kipaji wa kiakili. Wana mtambo mdanganyifu wa kupigia kura, kuwapa mmoja. Mungu sikuzote hukuacha upate shauku za moyo wako. Sasa, mmeipata. Mtafanya nini nayo?

⁹¹ Wakati hao wote walipokuwa wakilia wapate Masihi, Mungu aliwatumia Mmoja. Lakini, mmoja alitaka jenerali, mmoja alitaka mtambo wenye elimu, na wote kadhalika, lakini Mungu aliwatumia Mtoto mchanga. Aliwatumia Mwokozi. Alijua walihitaji Mwokozi.

⁹² Vipi kama Urusi ilipata masihi wao leo hii? Tungefanya nini? Mnaona? Mungu anajua jinsi ya kumleta.

⁹³ Vipi kama watu siku hizi... ambao wanaomba kwa ajili ya Masihi. Nasi tunaombea kitu fulani kikuu kutukia. Tunaomba. Sisi Wapentekoste tunaombea kitu fulani kikubwa kitukie. Nashangaa ni nini kingetukia kama kweli kilitukia? Na labda Yeye huyajibu maombi yenu nanyi hamjui. Wala hamtalipokea Hilo kama Yeye aliyajibu. Halingetukia katika rangi mliyoombea. Hivyo ndivyo wamefanya daima. Na kama Hilo likitukia tena, Hilo lingekuja katika rangi iyo hiyo. Lingekuja kwenye kifurushi kile kile. Linaenda moja kwa moja juu Yake!

⁹⁴ Kwa hiyo, Mungu hushughulika na mtu binafsi. Hakujishughulisha na Israeli wote siku hizo. Hafanyi hivyo. Alikuwa akimshughulikia Mvulana huyu wa Kiyahudi. Mnaona? Halihi kwa njia ambayo tunalitaka lije.

⁹⁵ Sasa, Myahudi huyu alikuwa ameona kitu ambacho—ambacho kilikuwa ni tofauti. Hicho ndicho kilichouvutia moyo wake. Kuna kitu alichokuwa—alichokuwa ameona, kilichokuwa ndani ya Yesu, ambacho watu wengine hawakuwa nacho. Alijua kuhani wake na marabi wake hawakuwa na kitu ambacho huyu—ambacho Jamaa huyu mdogo alikuwa nacho, aliyeitwa Yesu, Ambaye watu waliamini kwamba ni nabii. Alikuwa ni Mtu tofauti.

⁹⁶ Walikuwa wamemwona rabi wake akisimama, na Mafarisayo wakibishania wazo lao, kwamba, ‘Kulikuwako na Malaika na roho.’ Nao Masadukayo wakaja na kuthibitisha, “Hakuna Malaika na roho.” Nao walikuwa na tofauti zao. Naye jamaa huyu mdogo, akanaswa hapo katikati.

⁹⁷ Ambapo, kanisa limenasiwa siku hizi, “Hivi inahitaji makundi ya kimadhehebu? Hivi inahitaji kundi la wanaume? Hivi inahitaji kundi la wanawake?”

Inahitaji mtu mmoja aliyejisalamisha kwa Mungu, kwa Neno Lake.

⁹⁸ Yesu Kristo alikuwa ni Mungu, aliyefanyika mwili apate kufa. Ambapo, Neno, Yeye na Neno walikuwa ni mmoja. Neno lingepitia tu Kwake. Hapana shaka hata kidogo.

⁹⁹ Mungu anajaribu kumpata mtu fulani, kupitia kwa nguvu zinazotakasa za Kristo, kujitolea kwa Neno hilo, ili kwamba Yeye pamoja na Neno wanaweza kuwa mmoja tena, ndipo Yeye anaweza kulitumia Neno Lake kupitia kwa mtu huyo.

¹⁰⁰ Lakini, mnaona, huyu—huyu jamaa mdogo aliona kitu fulani ndani ya Mtu huyu, kilichokuwa tofauti na watu wengine. Alijua kulikuwa na tofauti.

¹⁰¹ Kwa sababu, wakati mmoja Yeye aliulizwa. “Mtu huyu hazungumzi kama watu wa kawaida. Kuna kitu fulani kumhusu Jamaa huyu ambacho ni tofauti. Hakuna mtu aliyewahi kunena kama huyu.” Kwa sababu, wakati Yeye aliponena, Mungu alikuwa hapo kujibu, yale aliyosema.

¹⁰² Kama nilivyosema mara nyingi, juma hili, mwanadamu angali ni mwanadamu. Wanamsifu Mungu kwa ajili ya yale aliyofanya, wakitazamia yale anayofanya, atakayofanya. Huyo ni sisi. Lakini unapuuza yale anayofanya. Daima, mwanadamu hufanya hivyo.

¹⁰³ Yesu alisema, “Mnadai kuwa wa—wana wa manabii. Nanyi ndio mliowaweka kaburini. Kisha mnayapamba makaburi yao.” Mnaona?

¹⁰⁴ Tuna—tunawazia yale Mungu aliyofanya kwenye Siku ya Pentekoste na kupitia wakati wa mwanzoni. Na halafu tunasema, “Mungu atakuja na kitu fulani kikubwa,” Na kitu cha kwanza mwajua, tunapita moja kwa moja (sisi) karibu nacho, wala kamwe hatutakijua. Historia daima hujithibitisha kuwa

kweli, na hujirudia yenyewe. Tunapita, tunaliacha lipite, wala hatulitambui.

¹⁰⁵ Sasa, kijana mwanamume huyu alikuwa ameona kitu tofauti. Aliona ya kwamba kulikuwako na tofauti katika huyu Yesu. Hakuwa kama watu wa kawaida. Alikuwa ameona yale Mtu huyo angeweza kufanya, ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yeye. Aliona ya kwamba maisha Yake, ingawa yalikuwa ni kinyume na mafundisho ya kanisa lake mwenyewe, lakini aliona, Mtu huyo, ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yeye.

¹⁰⁶ Kama vile Petro alivyosema, baadaye, kwenye Siku ya Pentekoste, alisema. Ama, ninaamini ilikuwa katika Matendo, mlango wa 3. Alisema, “Enyi watu wa Israeli! Yesu wa Nazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu, kwa maajabu na ishara aliyofanya! Mnaona! Ninyi kwa mikono ya watu wabaya...” Yeye alikuwa akikishtaki kizazi hicho kwa kumkataa. “Ninyi kwa mikono ya watu wabaya mmemsulubisha Mfalme wa Uzima.”

¹⁰⁷ Sasa, tunaona sasa ya kwamba tunakuja, katika wakati wetu. Na mwalimu yeyote wa Biblia anajua ya kwamba wakati wa mwisho, wa Kipentekoste, ni Laodikia. *Laodikia* maana yake ni “mwanamke,” katika Kiyunani, wakati ambapo wanawake watachukua mamlaka.

¹⁰⁸ Sina chochote dhidi ya wanawake, mradi tu wanakaa mahali pao. Kama Mungu angaliweza kumpa mwanamume kitu chochote chema zaidi, angalimpa. “Lakini wakati mwanamke anapoondoka mahali pake, yeye ni maji damuni mwa mume.” Sulemani alisema hivyo. Yeye ndiye mwenye hekima kuliko wote tuliypata kuwa naye.

¹⁰⁹ Lakini ni wanawake katika siasa. Hivi, miaka ishirini na mitano iliyopita, Bwana hakunipa ono lililoonyesha ya kwamba wanawake, kwa kuruhusiwa kupiga kura, wangemchagua—wangemchagua huyu riki tuliye naye hapa juu sasa, Ahabu mamboleo akiketi kule huku Yezebeli akiipindua shingo yake? Nanyi wanawake mnajipamba kimitindo vivyo hivyo, kwa kuwa yeye ndiye mama mtindo wa ulimwengu.

¹¹⁰ Kuna kufanana kwingi na—na Israeli, mwajua. Waliingia na kuiteka nchi, na kuwafukuza wenyeji, na kuweka hapo mfumo wao wenyewe. Na—na vivyo hivyo ndivyo Marekani ilivyofanya, tuliwasukuma nyuma Wahindi na kuweka mfumo wetu. Israeli ilikuwa na watu mashuhuri miongoni mwao. Walikuwa na kama vile Sulemani, na—na Daudi, na mashujaa wakuu. Tulikuwa na watu mashuhuri, Washington na Lincoln. Lakini hatimaye kukaja kitu kwenye kiti cha enzi ambacho, kupitia siasa, kimeletwa humo ndani. Na haikuwa Ahabu. Yeye alikuwa ni jamaa mzuri kweli, yeye binafsi. Lakini, yule mwanamke nyuma yake!

¹¹¹ Mnajua, Biblia inasema jambo lilo hilo, katika siku za mwisho hapa? Nanyi, huku mkizipenda siasa zenu, ninyi Wanademokrasia, mkiupenda msimamo wenu wa kisiasa zaidi ya mlivyoipenda Biblia yenu na Mungu, nanyi mkamchagua huyo. Mimi si Mripablikani. Mimi ni Mkristo. Nipo hapa kwa ajili ya jambo moja. Nena kuhusu kuuza haki za mzaliwa wa kwanza, tumeziuza. Hakika, mmeziuza. Na sasa mmekipata, mtafanya nini nacho? Iliwabidi kufanya hivyo, kuyatimiza Maandiko haya, nao watu waliona jambo hilo.

¹¹² Sasa angalieni, sasa, kanisa tajiri la Laodikia. Yesu anafunua, katika Ufunuo 3, anaupa wakati huu, wakati huu wa Laodikia wa Kipentekoste, nafasi ile ile ambayo tajiri huyu alipewa, ile ile. Maana, Laodikia, “Kubisha mlangoni,” kulionyesha ya kwamba maisha yetu ya kimadhehebu yalimweka Kristo nje. Kwa sababu, Kristo ni Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu,” na Neno lingali ni Mungu. Nalo Neno lilitolewa nje, kwa ajili ya mfumo wetu wa kimadhehebu.

¹¹³ Hiyo ndiyo sababu nipo hapa pamoja na hawa Wafanyabiashara. Mungu na awasaidie, ili kamwe wasiunde dhehebu. Lakini hamko mbali nalo. Ninyi kumbukeni tu hilo. Ninawapenda, nanyi mnanipa mahali, na hapa pamekuwa ni mahali pa huduma yangu. Lakini ninaliona likija. Maandishi ya mkono yako kwenye ukuta. Sasa, msifanye hivyo. Mtachukua mchafuko ule ule hao wengine waliochukua. Ibilisi amekuwa akijaribu kumwua kiongozi wenu kwa muda mrefu. Kama akiweza kumwondosha, jambo fulani litatukia. Ni wanadamu tu. Hawana budi kuwa na mawazo yao wenyewe ya jambo hilo. Mliweka mkataba hapa si muda mrefu uliopita katika gazeti lenu. Haikuwapasa kufanya hivyo. Hiyo inawatambulisha kama dhehebu. Sisi, sisi ni kundi la ndugu, ambao, haijalishi mtu huyo anaamini nini, tunashiriki, tukijaribu kumpata. Taa yenu na—na iwake. Yeye ataiona nuru.

¹¹⁴ Hudson Taylor alisema, sio muda mrefu uliopita, kwamba kulikuwako na mvulana mmishenari aliyekuja, kasema, huko India, kasema, “Bw. Taylor, ndio kwanza nimpokee Kristo.” Akasema, “Niende sasa na kupata Shahada yangu ya Sanaa, na—na kadhalika, na kujifunza?”

¹¹⁵ Akasema, “La. Nenda, ukashuhudie.” Kwa hiyo ninafikiri hilo ni wazo jema. Mnaona? Tunajaribu. . .

¹¹⁶ Mnaona, ukifanya hivyo, utajizungusha uingie katika kitu fulani. Ukitoka hapa nje na—na kuingiza programu nyingi za elimu, zinamtoa Mungu moja kwa moja nje.

¹¹⁷ Unapopata madoido, Mungu hapendi madoido. Hollywood imejaa madoido. Hollywood hung’aa; Injili humeka. Kuna tofauti chungu nzima kati ya kung’aa na kumeka. Hollywood hung’aa kwa taa na tabaka, nayo Injili humeka katika

unyeyekevu. Tofauti kubwa mno. Mnaona? Mnaona? Sasa, hamna budi kukumbuka hilo, ndugu zangu na dada zangu. Msi—msing'ae. Meken!

¹¹⁸ Sasa, tunaona, jamaa huyu kijana, alipewa nafasi hii ya kufanya jambo hili. Naye—naye... Akaikatalia mbali kwa sababu ilikuwa na gharama kubwa mno.

¹¹⁹ Na mimi—mimi nafikiri hilo ni jambo lile lile siku hizi. Sisi, hatutaki, hatutaki kukubali sasa, hatutaki *kusema* ya kwamba hatutaki, lakini maisha yetu yanathibitisha hilo. Hayo yanathibitisha hilo. Hiyo ni kweli kabisa.

¹²⁰ Lakini La—Laodikia ilimweka nje ya kanisa ambapo alikuwa akibisha, mnaona, akijaribu kurudi ndani. Nayo Laodikia ilimweka nje kwa sababu kwamba wao—walikuwa ni matajiri. Hawakuwa na haja ya kitu. Walikuwa ta—tajiri tu walivyoweza kuwa. Na kwa hiyo walisema, “Sisi ni tajiri. Hatuna haja ya kitu.”

¹²¹ Naye Mungu akasema, “Ninyi ni uchi, maskini, wenye mashaka, vipofu, wala hamjui.” Hiyo ndiyo shida, wakati hawajui.

¹²² Kama mtu yuko hapa nje mtaani, katika hali hiyo, uchi na kipofu, vema, karibu mtu yeyote aliye na moyo wa kibinadamu angemwendea mtu huyo, aseme, “Bwana, uko uchi. Uko hapa nje. Umeninii, umeanikwa. Basi karibu ndani.”

¹²³ Lakini kama mtu huyo aligeuka, akasema, “Sasa, wewe shika lako.” Mnaona? Sasa, utamfanyia nini jamaa huyo?

¹²⁴ Na hapa, wakati kanisa linapowazia ya kwamba lime—limevikwa sana, katika ninii yake...ni, katika haki yake ya kujibunia, mpaka u—unafikiri... Nawe unaanza kuwaletae Neno. Unasema, “Hilo ni kinyume na kanuni yetu ya imani.” Kitu gani? Uliuza, basi, haki yako ya mzaliwa wa kwanza. Wakati, badala ya kuwa na madoido, tunapaswa kuwa tukimeka.

¹²⁵ Badala ya kuwa na mia tano ama mia sita, wowote wale walio hapa kwenye kiamshakinywa... Hiyo ni sawa. Sina kitu dhidi yake. Ni—nipo hapa tu katika Jina la Bwana Yesu. Badala ya hilo, kunapaswa kuwe na kumeka miongoni mwetu, kwa Roho Mtakatifu. Labda kuna dazani moja tu, wanaomeka katika uzuri wa Bwana, Bwana Yesu angekuwa juu yetu sana mpaka mmeko wa Bwana ungekuwa ndani yetu.

¹²⁶ Lakini tunataka kung'ara, wafuasi wengi zaidi. Mnaona? Kanisa daima limehesabu uanachama. Mungu huhesabu tabia, sio uanachama.

¹²⁷ Kama nilivyosema juma hili, Elieza alitoa jasho, akijaribu kuipata tabia. Ndipo alipompata Rebeka, basi alikuwa na wakati mgumu sana kumfanya asimame kimya mpaka aweze kumvisha nguo.

¹²⁸ Hilo ni jambo lile lile na kanisa. Tunapata ile tabia katika kanisa la Kipentekoste. Lakini, kulivalisha nguo, na ukijaribu kusema jambo juu yake, basi kila mtu anainuka, “Hatutalivumilia tena. Hatutaki hili.” Mnaona? Mnaona, unapokuwa na tabia ya kufanyia kazi, lakini basi hu—huwezi kuwafanya wasimame muda mrefu kutosha, kuwarejesha ambapo waliangukia wakati mmoja.

¹²⁹ Ninyi, kanisa la Kipentekoste, mlitoka moja kwa moja kutoka katika umadhehebu. Hiyo ndiyo sababu ya Mungu kuwatoa, ilikuwa ili muwe Kanisa Lake. Mlifanya nini? Mligeuka moja kwa moja, mkarudi moja kwa moja katika kitu kile kile mlichotoka kwake, “kama mbwa kwenye matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwake.” Watu walifanya jambo lile lile. Na sasa hakuna tofauti kubwa ndani yenu. Mnaona?

¹³⁰ Sasa, natumaini hamfikiri ninajaribu kuwa mbaya ama fidhuli. Nimetumwa tu hapa. Huenda siku zangu ni chache. Ninasimama katika Jina la Bwana Yesu, kuwaambia yaliyo Kweli. Yazingatieni Maneno yangu, kama hayatatimia. Mnajaribu kung’aa. Acheni. Meken.

¹³¹ Sasa, kanisa tajiri la Laodikia limefanya jambo lile lile alilofanya yule kijana mtawala tajiri, kwa sababu gharama ilikuwa kubwa mno. Kamwe asingalilikubali Neno la Bwana, kwamba afanye nini. Afadhali achukue njia yake na madoido ya siku hizo, maana alikuwa na pesa nyingi, naye angeweza kutoka aingie kwenye mashirika ya—ya ninii—ya watu na—na kuishia wakati wake.

¹³² Vema, hivyo ni karibu vile tumefikia. “Tunaweza kuwa dhehebu kama hao wengine.” Na Pentekoste si dhehebu. Ni tukio. “Tunaweza kuwa *hiki, kile* ama *kinginecho*. Sisi ni kama tu hao wengine.” Nyinyi, mnapata wafuasi wengi zaidi, bali mna nini mnapowapata. Mnaona? Haiwapasi kufanya hivyo. Hilo ni kosa. Mnafanya nini? Mnafanya kosa lile lile la kijinga ambalo kijana huyu tajiri alifanya. Mnaona? Naam. Walimtoa nje kwa sababu ya kupenda kwao ulimwengu.

¹³³ Sasa, hebu na tuwachunguze baadhi ya watu hawa huko nyuma, na yale waliyofanya. Na hebu tuangalie ninii . . . mahali tulipo leo hii.

¹³⁴ Na sasa mtu fulani alisema, sio muda mrefu uliopita, kama nilivyowaambia. “Ati nini? Wewe, ukiwa mhubiri, kwa nini unaambatana na hao wafanyabiashara?” Nikawaambia nilikuwa mwuzaji wa hakikisho la Uzima wa Milele. Kwa hiyo, hiyo hapo.

¹³⁵ Na hiyo ndiyo Yesu alikuwa akijaribu. Kijana mwanamume huyu alikuwa ameona kitu ndani Yake, sasa, kilichokuwa tofauti, na alijua Yeye alikuwa na Uzima wa Milele. Kwa hiyo

badala ya kumwendea rabi wake, alimjia Mtu huyo ambaye aliona alikuwa ni Neno la Mungu hasa lililothibitishwa.

¹³⁶ Mungu na Kristo walikuwa ni mmoja. Maana, Kristo alisema, “Si Mimi ninayezitenda hizi kazi, ni Baba Yangu.”

¹³⁷ Basi kama vile nilivyohubiri huko katika Central Assemblies, ama First Assembly, hivi majuzi usiku, jinsi ambavyo asili kuu ya Mungu ilivyomdhihirisha Yesu. Mnaona, asili zingine zote zilikuwa zimeanguka. Yeye asingeweza kumchukua nabii, kwa sababu alizaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili, naye alikuwa ni asili iliyoanguka. Lakini Mungu, katika upendo Wake, alimtoa Mmoja asiye na dhambi. Na hivyo basi Huyu alikuwa ni mkamilifu sana pamoja na Baba, mwili tu uliokuwa hapa, ulioitwa Mwana, hata Neno lilikuwa ni Yeye. Yohana analielezea katika mlango wa kwanza. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili.” Mnaona?

¹³⁸ Njia sasa, “Neno la Bwana liliwajia manabii,” bali Yesu alikuwa tofauti na hao. Yeye alikuwa ni Neno. Mnaona? Nabii angeweza tu kusema yale—yale yaliyowekwa kinywani mwake kusema. Lakini Yesu alikuwa Neno hilo, hata Neno lote la Mungu lingeweza kupitia Kwake. Bila... Na Yeye angeweza kuumba, kukomesha upepo na mawimbi, na chochote zaidi, kwa sababu ilikuwa ni Mungu, daima katika Neno.

¹³⁹ Sasa Mungu anajaribu kutafuta Kanisa ambalo anaweza kudhihirisha Neno Lake kupitia. Mnaona, Mungu huliangalia Neno Lake, apate ku—ku—kulithibitisha.

¹⁴⁰ Basi anawezaje kulithibitisha Hilo wakati tunakana kwamba Hilo ni Kweli. Mnaona?

¹⁴¹ Kwa hiyo, makuhani hawa, pamoja na neno lao, ingawa katika njia yao wenyewe ya kuwazia walikuwa sahihi kabisa; Mafarisayo, Masadukayo, Waherodia, na chochote walichokuwa. Imefikia wakati huo tena. Mnaona? Kila mmoja katika mawazo yake mwenyewe, wanafanya tu yaliyo sahihi, kama ilivyokuwa katika siku za Waamuzi.

¹⁴² Vema, kuna mkataa mahali fulani, na mkataa huo ni Neno la Mungu, maana Yeye alikuwa ni Neno.

¹⁴³ Sasa, tunaona ya kwamba waliyapenda mambo haya kuliko walivyompenda Mungu. Biblia ilisema wangeyapenda. Sasa tunaishi katika siku hiyo. Sasa, kama unabii ulisema jambo fulani, tunalionika likitukia, ndipo ha—hatuna budi kujua kosa letu lilipo. Hatuna budi kujua mahali inapotubidi kupita. Sasa, kitabu cha Ufunuo, mlango wa 3, kinafundisha hili, ya kwamba tungekuwa katika Wakati huu. Basi sisi hapa.

¹⁴⁴ Sasa, vipi kuhusu baadhi ya hao, kama tungalikuwa na wakati kukaa kwenye hili muda mrefu? Lakini hebu

tuharakishe, tupate kumaliza, maana ninapaswa kuwa nimeondoka saa moja iliyopita.

¹⁴⁵ Lakini angalia hapa. *Hili* ndilo la kwanza, hakika, Neno la Mungu. Sasa hebu tuchunguze baadhi ya wamiliki wa hati ya mkataba wa Uzima huu wa Milele, tuone kile ilichowagharimu, wamiliki wa Neno la Milele.

¹⁴⁶ Sasa, “Ndugu Branham, ulisema, ‘Neno la Milele.’” Naam, bwana.

¹⁴⁷ Milele kamwe haikuanza. Milele haina mwisho. Nalo Neno ni wazo lililotamkwa. Hayo yalikuwa ni mawazo ya Mungu kabla hapajakuwapo na ulimwengu, wala nyota, mwezi, wala chochote kile. Hayo yalikuwa ni mawazo ya Mungu, yale Yeye angefanya. Ndipo alipolinena Neno, ni la Milele, kwa sababu hawezi kutoa chochote ila kitu cha Milele. Hivyo ndivyo tu tulivyo na Uzima wa Milele, ni wakati tumeondolea mbali maisha haya yaliyopotoshwa na kuupata Uzima wa Milele. Huo ni Mungu, *Zoe*, Neno moja kwa moja ndani yako. Halafu Neno huja moja kwa moja kupitia wewe na kujidhihirisha Lenyewe.

¹⁴⁸ Na hilo ndilo jamaa huyu tajiri aliloona, ya kwamba huyu Yesu angeweza kusimama pale na Yeye aliyatambulisha Maandiko.

¹⁴⁹ Yesu alisema, Mwenyewe, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayosema Mimi ni Nani. Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Mnaona? Lakini walikuwa wameliweka katika kanuni za imani sana, kama vile tumefanya leo hii, hata wasingeweza kuliona Hilo.

¹⁵⁰ Sasa angalieni. Nuhu aliitwa na Neno la Mungu, naye akawekeza katika Mungu, Neno la Mungu la ahadi. Yeye alikusudia, haijalishi jinsi—jinsi ulivyoonekana ni mbaya, na jinsi gani walimwengu waliobakia hawakuliamini, Nuhu alifanya huo uwekezaji. Aliwekeza katika Mungu, ingawa ilikuwa ni kinyume na sayansi. Tungedumu hapo muda mrefu.

¹⁵¹ Bwana akipenda, ninataka kuhubiri juu ya “kuhesabu kinyumenyume,” Jumapili alasiri, tuone mahali tunapoishi. Vema.

¹⁵² Angalieni, yeye... Ilikuwa ni kinyume na imani yao ya kidini. Ilikuwa ni kinyume katika utafiti wa kisayansi wa siku hiyo, kwamba kulikuwa na mvua yoyote angani. Kamwe haikuwa imenysha. Kwa hiyo, basi, ilimbidi ku—ku—kuchukua msimamo, na kuwekeza. Naye akafanya hivyo, katika ahadi ya Mungu. Shetani alimjaribu kwa kila njia aliyoweza, hata hivyo akaushikilia uwekezaji wake. Nao ukaleta faida, wakati wa mwisho, kwa kuyaokoa maisha yake.

¹⁵³ Sasa enyi wafanyabiashara, mngeweza kuwekeza kitu gani kizuri kuliko hicho, kwenye wakati wa mwisho mahali tulipo? Na hata sayansi yenyewe sasa inakuja huku, iko pamoja nasi, na inatwambia kwamba ni kweli, “usiku wa manane umekaribia kupiga.” Vema, vitu vyetu vikubwa vitatufaidi nini? Dhehebu letu kubwa linafaa nini, milioni moja zaidi, na kadhalika namna hii, na kuyajenga namna hiyo, wakati Uzima wa Milele ukingojea huko ng’ambo? Nasi tunayo nafasi, na tumealikwa kumpokea huyu Kristo, ili—ili Mungu aweze kukuchukua na kukuweka kwenye Neno Lake kufikia mahali ambapo, mpaka unaponena, mambo ambayo—ambayo yametangulia kuonekana, na kubashiriwa, na kadhalika, yangeweza kutenda kazi moja kwa moja kupitia kwako, kila wakati vivyo hivyo hasa. Hayashindwi kamwe. Hayawezi kushindwa.

¹⁵⁴ Loo, unasema, “Nimeona hilo likijaribiwa.” Naam. Ninajua. Pia umeyaona yakishindwa, ambapo pana uigizaji.

¹⁵⁵ Lakini unapooni kitu kilicho halisi, hakiwezi kushindwa, maana ni Mungu. Naye Mungu huyaweka mambo haya kama mfano, ili wengine waweze kuona.

¹⁵⁶ “Jinsi gani,” mnasema, “linakujaje? Kwa kufunga usiku kucha?” Hilo ni zuri. “Mkutano wa maombi ya usiku kucha?” Huo bado ni mzuri.

¹⁵⁷ Lakini utii kwa Neno ndipo linapopitia, kulitii Neno. Mnaona? Vema.

Sasa, lilileta faida, kwa kuyaokoa maisha yake.

¹⁵⁸ Hebu—hebu tuuchunguze uwekezaji mwingine. Ambao, mtu jina lake Danieli, alijua. Alikuwa akienda . . . Kanisa lilikuwa likishuka kwenda miongoni mwa watu wa ulimwengu, kwa hiyo alijua ya kwamba jambo hilo lote lingeelekea huko.

¹⁵⁹ Hilo ndilo hasa tunaloona sasa. Pentekoste imetoka ikaingia miongoni mwa ulimwengu.

¹⁶⁰ Nawazia juu ya Ndugu Glover anayeketi hapa. Ninaamini yeye yuko na watu wa Foursquare. Nami nilikuwa nikizungumza siku moja na Ndugu Shakarian na—na mtu huyo mwungwana, Ndugu McPherson, Ndugu Rolf McPherson. Tulikuwa tumeketi ndani, nao walikuwa wakizungumza.

¹⁶¹ Nilikuwa nimeenda kwa mtu fulani ambaye alikuwa ameshirikishwa katika namna fulani ya m—mvua ya vuli ama kitu fulani. Basi mmoja wa walimu alikuwa akinikemea kuhusu jambo hilo, kwa nini “nilikuja kwenye hilo Hekalu kwanza? Na halafu baadaye . . . Ama, nikae mbali na hilo.”

¹⁶² Nikasema, “Vema, sasa, kumbukeni tu, ya kwamba Lutheri ilikuwa mvua ya vuli kwa Katoliki. Naye Wesley alikuwa mvua ya vuli kwa Luther. Nayo Pentekoste ilikuwa ni mvua ya vuli kwa Wesley. Bibi McPherson alikuwa mvua ya vuli kwa Pentekoste. Yote ni mvua za vuli. Watoto hupata njaa.

Wasipopata chakula, watakula kwenye pipa la takataka. Lakini Mungu atatoa Chakula ikiwa tu wako tayari kukila.”

¹⁶³ Basi Bibi McPherson, yule mama mwungwana, alisimama na kusema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham.” Ametoka kwenye asili nzuri, ya Kipentekoste. Alisema . . .

¹⁶⁴ Nilimwambia Rolf, “Mradi tu hapa, kwamba Hekalu letu limeenda mbali sana na kile kitu ambacho Bibi McPherson alikuwa akiwaambia habari zake.”

¹⁶⁵ Nao wakaanza kujifanyia madaktari, na Ph.D. na LL.D., basi ni kitu gani ila lundo la mchanga wenye thamani ya dola milioni moja, na mzigo wa fedha nyingi usio na faida mkononi mwao? Kile mnachohitaji ni kurudi kwenye kanuni na uaminifu wa Injili, kukirudia kile kitu halisi cha kipentekoste ambacho kinazaa Kristo katika maisha ya watu. Hiyo ni kweli. Mnaona? Sisi, tunayaondokea hayo mambo yaliyo halisi.

¹⁶⁶ Naye tajiri huyu hapa aliona hilo. Naye alijua ya kwamba Yesu alikuwa nalo. Ndipo akaulizwa, “Ninawezaje kuupata?” Naye Yesu akamwambia, nayo gharama ilikuwa ni kubwa mno.

¹⁶⁷ Hivyo ndivyo Assemblies of God, Foursquare, Umoja, na hao wengine wote, wanavyofanya. “Jambo hilo, gharama yake, ni kubwa.”

¹⁶⁸ Turudini tu kwenye huo uaminifu wa Neno, tuliamini Hilo, ili Mungu aweze kujithibitisha Mwenyewe.

Mnasema, “Yeye atafanya hilo?” Hakika. Yeye hulifanya.

¹⁶⁹ Maisha yako yataangaza kwa sauti kubwa zaidi kuliko vile ushuhuda wako ungaliweza kutoa. Maisha yako yanatoa sa—sauti kubwa sana hata watu hawaelewi ushuhuda wako. Hiyo ni kusema, palipo, uaminifu na utakatifu. Watu watano wazuri, waliojazwa na Roho kweli, watafanya mengi zaidi katika Phoenix kuliko wafuasi wote tulio nao, kama wamejiweka wakfu kwa Mungu, katika maisha ya uaminifu, maana Mungu atalipeleka Neno Lake kule na kulithibitisha Hilo kwamba ni Kweli. Ndipo muda si muda mwajua, mambo yanatendeka. Kwa hiyo mnaninii tu. . . Hamwezi kulizima.

¹⁷⁰ Stefano alikuwa ndiye yote Yeye aliyohitaji, kwa mahakama ya Wazee, ile halmashauri asubuhi ile, ilikuwa ni mtu mmoja ambaye angeweza kusimama pale akiwa na Kweli moyoni mwake, ambapo alijua. Na Hilo lilisema, “Alinawiri kama Malaika.” Mnaona, alijua yale aliyokuwa akizungumzia. Neno lilikuwa nyuma yake. Alilielezea, kasema, “Baba zetu huko Mesopotamia,” na kadhalika, na kuwaelezea Hilo. Kasema, “Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyoni, masikioni! Sikuzote mmempinga Roho Mtakatifu. Kama Baba zetu walivyofanya, baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo.” Mnaona? Mtu huyo alijua yale aliyokuwa akizungumzia. Yeye aliyaweka Maandiko huko nje, ndipo ikamgharimu uhai wake.

Lakini alikuwa ni mwaminifu, kwa sababu alijua yale aliyokuwa akiamini, naye Mungu akayathibitisha.

¹⁷¹ Basi walipokuwa wakimpiga mawe maskini jamaa huyo hata kufa, yeye alisimama na kusema, “Namwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu,” wakati mabonge yalipokuwa yakiuponda maskini ubongo wake utoke nje. Hata hivyo, Mungu... Siamini alihisi pigo lake hata kidogo. Mungu alimkumbatia kwa mikono Yake, kisha akampembeza katika kitanda kidogo cha amani mpaka akaenda kuwa pamoja na Mungu. Yeye alijua. Yeye, alijua, na Mungu alikuwa akithibitisha pale. Hata katika mauti yake, alimwona Yesu amesimama mkono wa kuume.

¹⁷² Danieli, akijua ya kwamba ulimwengu ulikuwa ukitaka kuingia kanisani, na uliingia. Lakini angalieni. Yeye alichukua moja ya hati hizi za mkataba wa Uzima wa Milele pamoja na Mungu, naye akakusudia moyoni mwake ya kwamba hatauharibu uwekezaji wake. Amina. Kanisa hilo, la hao Wafanyabiashara, laiti ninyi watu mngaliuchukua tu msimamo huo, laiti mngalishughulikia tu upande huo, mafanikio hayo, kwamba hamtauharibu uwekezaji huu ambao mmefanya katika Kristo, kwa mambo ya ulimwengu, na madoido.

¹⁷³ Mbona, kitu chochote kinaweza kung’aa na kumeka, basi ni kitu gani kinachokiendea? Tumbili. Hiyo ni kweli. Tumbili daima huendea kitu kinachometameta. Mnaona? Hiyo ni kweli. Angalieni, ndivyo tulivyo. Hilo ndilo ninalomaanisha. Mnaona? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Ibilisi atawafanya kuwa tumbili, akiweza. Anajaribu kuwafanya muwazie ya kwamba mlitokana na mmoja, hata hivyo, kwa hiyo, pamoja na mifumo yao ya elimu, na mambo ya siku hizi. Bali sivyo ilivyo. Hiyo ni kweli.

¹⁷⁴ Danieli alikusudia moyoni mwake ya kwamba hatajichafua na ulimwengu. Alikuwa anaenda kudumisha utaratibu ambao Mungu alikuwa ameandaa, zile amri za Mungu.

¹⁷⁵ Kwa nini ninyi wanawake na wanaume msiweze kufanya jambo lile lile? Lakini Marilyn Monroe ama mtu fulani walizikata nywele zao, halafu mke wa mhubiri fulani akafanya jambo lile lile, nanyi mnafikiri mna haki ya kufanya hivyo. Hilo haliwaachilii kutoka kwa Neno la Mungu.

¹⁷⁶ Nanyi wahubiri mnawaacha wake zenu wawaongoze. Ni aibu jinsi gani! Ni—ni—ni neno la jinsi gani, la kuwa *mwanamume*. “Mtumishi wa Kristo asiyeweza kuiongoza nyumba yake mwenyewe, ataongozaje nyumba ya Mungu?”

¹⁷⁷ “Vema,” mnasema, “Ndugu Branham, hayo, hayo ni mambo madogo tu.” Vema.

¹⁷⁸ Hebu na tuyanyoshe mambo yaliyo madogo, ndipo tuliendee jambo kubwa. Mnaona? Ndipo tutazungumza juu ya Roho Mtakatifu, na ma—na mambo ya jinsi ya kupokea karama za Kiungu.

179 Kama vile mtu fulani wa . . . alitoa tamshi hili fidhuli, lakini niliambiwa, kasema, “Daima unawakemea hao wanaume juu ya *hili*, na kuwaacha wake zao wafanye *hivyo*, na kuvaa kaptura, na huko nje mitaani, na—na huku kuvaa kizinifu kweli, kutamanisha kizinifu.”

180 Linazungumziwa kwa nadra sana kutoka mimbarani. Wanafikiri tu hilo ni jambo la kawaida. Tunahitaji mtu wa Mungu, mtu fulani atakayesimama pale na kulihukumu jambo hilo.

181 Wao wanasema, “Vema, unapaswa kuwafundisha hao wanawake jinsi ya kupokea karama za kiroho. Uwafundishe jambo kubwa.” Mtu fulani mashuhuri aliniambia hilo. Akaweka mikono yake juu yangu, kasema, “Nitakuombea.” Akasema, “Kamwe usininii. . . Ondokea jambo hilo.” Kasema, “Ukweli ni kwamba, Mungu alikutuma ukawaombe wagonjwa.”

182 Nikasema, “Kama Mungu alimtuma mtu, Yeye alimtuma pamoja na Injili yote kama kwa vyovyote Yeye alimtuma.”

Akasema, “Vema, utaumiza huduma yako.”

183 Nikasema, “Huduma yoyote ambayo Neno litaumiza inapaswa kuumizwa.” Hiyo ni kweli. Hakika.

Akasema, “Vema, watu watakukataa.”

184 Nikasema, “Sina vipindi vya redio na vipindi vya televisheni kugharamia. Niko huru katika Kristo. Mimi huhubiri tu yale anayoniambia pale.” Amina. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] “Sihitaji matoleo.”

185 Sihitaji chochote ila neema zaidi ya Mungu, kusimama na kusema Kweli; na kutopatana juu ya Neno la Mungu, kupiga kona yoyote ama mambo ya udanganyifu, ili tu kumsaidia mtu fulani, kuwachukua na kuwafanya maradufu wana wa kuzimu kuliko walivyokuwa hapo awali. Waambie Kweli. Ndipo nitakaposimama pale mwishoni mwa safari yangu, ninaweza kusema, “Hakuna damu ya mtu yeyote juu yangu.” Hiyo ndiyo shauku yangu. “Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.” Sasa, unawezaje kuwafundisha watu—watu aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?

Kasema, “Watu wanadai wewe ni nabii, mwonaji.”

Basi nikasema, “Sidai hilo.”

Kasema, “Lakini watu wanalidai. Unapaswa kuwafundisha mambo yenye kilindi.”

186 Nikasema, “Unawezaje kuwafundisha mambo ya kilindi wakati hata hawatajifunza ABC zao?”

187 Daima mwamini Kristo: ABC. Hiyo ni kweli. Bali hawatafanya hivyo. Kwa hiyo utawafundishaje kipimo cha kipeo cha pili na kadhalika, hisabati halisi ya Mungu? “Unaonaje maono? Mambo haya yanatendekaje?” Jamani!

¹⁸⁸ Unataka kuvuta kitu fulani kidogo, ambacho, kundi dogo la kimadhehebu linaloonekana kitu kidogo kwako, na maskini kitu fulani kiangavu kinachonawiri unachokimbilia. “Na kama ilitokea niliendee—niliendee Neno, ama kitu kingine namna hiyo, kiongozi wangu wa jimbo ataniondoa, ama askofu wangu atanitupa nje.” Mbona, kama ukija kwa Mungu, utatupwa nje, hata hivyo. Kwa hiyo tofauti ni nini? Afadhali niwe. . . Kama ukitupwa nje, unatupwa ndani. Kwa hiyo jambo ndilo hilo. Mnaona? Mnaona?

¹⁸⁹ Kuna mambo matatu. Mungu sikuzote hufanya kazi katika tatu. Tunajua hilo. Yeye hukamilika katika tatu. Kumbukeni, katika siku za Nuhu, waliingia *ndani* ya safina. Na katika siku za Sodoma. . . Yesu alikuwa akizungumza juu ya haya mawili. Siku za Sodoma, walitoka *nje*. Waliingia *ndani*, katika wakati wa Nuhu. Walitoka *nje*, katika—katika siku za Sodoma. Halafu basi kwenda *juu*, katika wakati huu. Naam. Kuingia ndani, kutoka nje, kupaa juu! Mnaona?

¹⁹⁰ Hilo ndilo tunalohitaji sasa. Tunahitaji shughuli ya kupaa juu. Tunahitaji kupaa juu kutoka kwa mambo haya na mambo ya kilimwengu ambayo yametufunga sana.

¹⁹¹ Danieli alikataa kujitia najisi. Angalieni, alikuwa akitaka kuliweka Neno hilo mahali ambapo Hilo lingeweza kububujikia, Neno. Lingefanya nini? Lilimshusha Malaika. Liliyalinda maisha yake. Hakujiharibu.

¹⁹² Wale wana wa Kiebrania walidhamiria. Walisema, “Hao wengine wote wanasujudia filimbi zikilia, na wakati maaskofu wanaposema, ‘Kanyaga.’ Na wanapiga makelele, ‘Kichura,’ wanaruka. Lakini,” akasema, “sisi hatutafanya hivyo. Huenda ukafanya hivyo. Unaweza kutuchoma kwa moto. Unaweza kutufukuza. Unaweza kufanya *hili*, ama *lile*, ama *linginelo*. Lakini hatutaisujudia sanamu yako, kwa vyovyote vile.” Mnaona? Hawakuwa wakienda ku—kutia unajisi kitega uchumi chao. Ilikuwa iwe ni Neno. Na, Neno, walikuwa wanaenda kusimamia. Basi wakati ulipowadia wa kufanya uamuzi, walikuwa wanaenda kusimama na Neno. Iliyaokoa maisha yao. Kulikuwa na Mtu wa nne huko chini.

¹⁹³ Kama kuna kitu tunachohitaji asubuhi ya leo, ni huyo Mtu wa nne, miongoni mwetu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hilo, sasa.

¹⁹⁴ Sasa, Petro, wakati mmoja, yeye alikuwa—Yeye alikuwa si kitu ila mvuvi. Alikuwa na biashara, mvuvi. Lakini mnajua nini? Yeye aliona kitu fulani katika Yesu Kristo, ambacho baba yake. . . Vema, mwajua, baba yake, Yona, alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa ni mvuvi.

¹⁹⁵ Nitafanya mchezo mdogo tu wa kuigiza hapa kabla hatujafunga, hiyo ni katika dakika chache zijazo. Sisi. . . Saa tano tu na dakika kumi. Tutajaribu kumalizia ifikapo saa tano

na nusu, kama mnaweza kuvumilia kidogo zaidi. Kwa hiyo, sisi, tutaendelea.

¹⁹⁶ Nami najua, huenda Yona alikuwa amemwambia mwanawe, katika mchezo mdogo tu wa kuigiza, wakati alipomweka yeye na Andrea pajani mwao. Huku nywele zake zenye mvi ziking'ara, baada ya siku kadhaa za kuvua samaki, ambapo iliwabidi kutumainia, kila siku, wapate riziki yao ya kila siku. Nami ninaweza kumwona yeye ameketi pale, akisema, "Mwanangu, sikiliza, Simoni. U—utakuja wakati. Sikuzote nilitaka kumwona Masihi. Nasi sikuzote tumeamini hilo, kwa sababu tumeahidiwa Mmoja. Lakini, sikiliza, Simoni, mwanangu. Kutakuwako na mambo mengi ya bandia yatakayoinuka," na yalikuwako, "kabla Masihi halisi kuja. Lakini," kasema, "utamjua Masihi huyu, Simoni, kwa sababu atakuwa sawasawa na Maandiko kikamilifu. Na hao wengine wote watampinga." Mnaona?

¹⁹⁷ "Lakini Masihi huyu atathibitisha, kwa sababu sisi ni Wayahudi. Tumefundishwa kuwaamini hao manabii. Maana, Bwana Mungu alitwambia, 'Akitokea mmoja wa kiroho miongoni mwenu, ama nabii, Mimi Bwana nitasema naye katika maono. Na yale asemayo yatatimia, nanyi mtajua ya kwamba mtu huyo ni nabii.' Naye Musa alitwambia ya kwamba Masihi wetu angekuwa ni nabii. Nanyi mwangalieni Yeye. Sasa, hatujakuwa na mmoja kwa mamia na mamia ya miaka. Lakini, mjue hilo."

¹⁹⁸ Baada ya mzee huyo mwungwana kuaga dunia. Basi siku moja Andrea alikuwa ameyumbayumba, akashuka kumsikia m—mtu akihubiri, ambaye alikuwa akitabiri juu ya Masihi ajaye. Ndipo baada ya kitambo kidogo, Masihi huyu akajitokeza jukwaani.

¹⁹⁹ Na sasa—sasa, Yohana, aliyekuwa akimtarajia, aliiona ishara ya Mungu ikishuka. "Yehova, yule Mungu aliyekuwa akinena kwa Sauti, na katika mfano wa hua, akishuka juu Yake, nayo Sauti ikisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.'" "Ninayependezwa kukaa ndani Yake," vile vile, geuza tu kitendo kabla ya kielezi. Mnaona? Sasa, "'Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake, ama kupendezwa ku—kuwa nikikaa ndani.' Yeye, Yeye ameniridhisha. Amefanya yale tu ni—ninayojua kwamba Yeye anapaswa—Yeye anapaswa kufanya, na yale niliyosema Yeye angefanya." Sasa, na wakati Petro alipokuwa amesimama, ama ninamaanisha . . .

²⁰⁰ Andrea, akisimama pale, aliona hilo. Kwa hiyo alimwona Yesu kesho yake, kasema, "Rabi, unakaa wapi Wewe?"

Akasema, "Njoo, uone."

²⁰¹ Kwa hiyo basi akaenda akamwambia ndugu yake. Baada ya kukaa pamoja na Yeye usiku kucha, kesho yake asubuhi alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi.

Basi kesho yake asubuhi, akaenda kumtafuta ndugu yake. Ndipo akamleta, akasema, “Njoo. Tumempata Masihi.”

²⁰² Ninaweza kumwazia Simoni akisema, “Sasa, ngoja kidogo tu. Mimi ni mvuvi mfanyabiashara hapa. Mimi ni—mimi ni Mfarisayo hapa. Mimi ni mfuasi wa kanisa lile lile baba yangu alikuwa ni mfuasi wake. Nami nimekuwa na upuuzi huu wote wa Masihi, kotekote.”

²⁰³ “Lakini ngoja kidogo, Simoni. Hivi unakumbuka mafundisho ya Neno le—letu? Unakumbuka yale... Ninajua umeona upuuzi huu wote. Lakini hivi baba hakututabiria ya kwamba upuuzi huu wote na madoido yangeibuka, bali huo haungekuwa ndio? Lakini tungejua Yeye angekuwa ni mtu wa Kimaandiko. Yeye angedumu na Neno kwa sababu Yeye atakuwa ni Neno.” Mnaona? Kwa hiyo kamwe wasingeelewa hilo.

Kwa hiyo Simoni anakaribia, na kusema, “Vema, nadhani nitaenda nikaone.”

²⁰⁴ Basi mara alipokuja Mbele ya Yesu...Sasa, alikuwa amepoteza siku nzima ya kuvua samaki, ya riziki yake ya kila siku. Alikuwa ni mfanyabiashara, mnaona. Na kwa hiyo akaja kwenye mkutano huu. Na katika jambo hili, yeye akakaribia.

²⁰⁵ Ndipo wakati Yesu alipomwona, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani Yake.” Mnaona? Tazameni. La, samahani. Nilimnukuu mtu mwingine.

²⁰⁶ Hivi ndivyo Yeye alivyosema. Alisema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.”

²⁰⁷ Ndipo Petro akachukua hati ya mkataba. Mnaona? Akawekeza papo hapo. Si kwamba tu Yeye alijua alikuwa ni nani, alimjua maskini yule baba mzee mtauwa ambaye alikuwa amemwambia yatakayotukia. Naye akaliona Neno limethibitishwa. Yule kijana tajiri mtawala huenda alikuwa amesimama, kuona jambo lilo hilo. Lakini Petro alikuwa tayari kuuza biashara yake na uanachama wake, na kuwekeza. Lilimfanyia jambo fulani.

²⁰⁸ Vipi kuhusu Nathanaeli? Alikuwa na kijisitu hiki kule nje, kama vile mlivyo navyo hapa Phoenix. Basi—basi siku moja alikuwa huko nje. Naye alikuwa ni mwanafunzi wa Biblia. Basi Filipo alipoona hili likifanywa, alimwendea na kumwambia, kasema, “Aisee! Tu—tumemwona Masihi Yule ambaye Musa alinena habari zake.”

Akasema, “Sasa!”

“Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.”

²⁰⁹ Kasema, “Sasa, chaweza chochote chema kutoka mahali kama hapo? Nimechunguza. Ati ulisema Yeye alikuwa ni nani?”

“Yesu wa Nazareti.”

210 “Nimemchunguza kila mmoja wa viongozi wetu, na hakuna mmoja wao ambaye amesema chochote kumhusu Yeye. Hatuna shule yoyote ya seminari alimotoka Yeye. La.”

211 Hivi mlijua, kotekote katika Biblia, manabii walioinuka, hatujui walitokea wapi? Hamna historia kwao. Waliingia tu jukwaani, kisha wakaondoka tu vivyo hivyo. Hawakuwa na ujuzi wowote huko nyuma mahali fulani. Walikuja kuwaleta watu waliokuwa wamelegea, na kuirejesha miisho hiyo na kuifunganisha katika Biblia tena. Mnaona?

212 Musa alitoka wapi? Mzazi mnyenyekevu. Tunajua tu mzazi wake, hatujui chochote kuhusu usuli wake.

213 Mwangelie Eliya. Hata hatujui baba na mama yake walikuwa ni nani; alijitokeza tu jukwaani.

Mwangelie Obadia. Waangelie hao wengine wote.

214 Mwangelie Amosi, tulinena habari zake hivi majuzi usiku. Hakuna anayejua mahali alikotoka. Alikuwa ni mchungaji. Hayo ndiyo yote tujayo. Alijitokeza tu jukwaani.

215 Hata hivyo, alipoimaliza kazi yake, kama yule Eliya mkuu, Mungu alimbeka kwa gari la kukokotwa hata Mbinguni. Mnaona?

216 Hatujui walikotoka. Hawana shule wala usuli. Mungu huwainua tu, kulirejesha hilo Neno. Nao hawana mshikamano wowote wa kimadhehebu kufunganisha kwake, na kusema huna budi kufanya *hili*, ama kuwafukuza.

217 Mwangelie hata Yohana Mbatizaji, yule nabii maarufu, hata katika ukoo wa kuhani, lakini kamwe hakwenda kwenye shule za baba yake. Iimpasa kumtambulisha Masihi.

218 Asingeweza. Mbona, kila mmoja alikuwa akisema, “Sasa, mwajua Dk. Jones hapa. Yeye ni mtu mzuri. Unajua unamtambua kama Masihi.” Asingeweza kushawishiwa na kundi la watu kama hao.

219 Yeye alienda nyikani, maana kazi ya—yake ilikuwa ni muhimu. Naye akakaa huko nje mpaka akasikia kutoka kwa Mungu. Na alijua kile Yeye angekuwa. Basi alipomwona Yeye akija, alisema, “Yule pale Mwana-kondoo wa Mungu aziondoaye dhambi za ulimwengu.” Hao wengine hawakuona kitu chochote. Lakini yeye aliiona.

220 Nathanaeli, kidogo alishangaa. Lakini alipopanda pale, alimwambia yale aliyokuwa amemwambia Petro. Kasema, “Sasa, unajua ya kwamba sisi ni wanafunzi wa Maandiko. Tunajua ya kwamba Masihi atakuwa ni nabii.”

221 Kwa hiyo, alipojitokeza jukwaani, mbona, alimwendea. Na Yeye akasema... Akapanda kwenye kusanyiko. Ndipo Yesu akamwambia, kasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Rabi, ulinijua lini Wewe?”

222 Kasema, “Kabla Filipino hajakuita. Ulipokuwa chini ya mti, katika mkutano wa maombi huko nje, nilikuona.” Ni macho ya jinsi gani!

223 Basi papo hapo yeye akawekeza. Alifanya nini? Papo hapo mbele ya rabi wake, kuhani, na kila kitu, yeye alikiri unafiki wake. Akaanguka miguuni pake... akatoka miguuni mwake, akapiga magoti, akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

224 Wakati, wengi wa hao watu wenye tabaka la juu walisimama pale, na taratibu zao zote na kadhalika, na kusema, “Mtu huyu ni Beelzebuli.”

225 Ndipo Yesu akawaambia, “Walikuwa wakikufuru, wakimwita Roho wa Mungu kitu kiovu. Mnaona? Hakika. Loo, jamani!

226 Maskini yule mwanamke kisimani, vipi kumhusu yeye? Bila shaka alikuwa na kitega uchumi. Wakati alipotoka huko nje, katika utovu wake wote wa uadilifu. Kanisa lilikuwa limemfikisha mahali ambapo hata hakujua mahali alipokuwa, na kwa hiyo akaingia kwa ukahaba tu; lakini moyo rahisi, mnyenyekevu.

227 Huenda hili likawa ni neno kubwa, nami ninawatakeni mlichukue vizuri. Yeye alikusudiwa Uzima wa Milele tangu zamani. “Wote alionipa Baba watakuja.” Ilimbidi kuja kuchota Maji, naye akayapata, bali si kutoka kwenye kisima cha Yakobo. Mnaona? “Hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba kwanza. Na wote alionipa watakuja. Nitamfufua tena katika siku za mwisho.” “Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wale ambao amewaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, aliwatakasia; ama, tayari, amewatukuza.”

228 Angalieni. Wakati Neno hilo, ishara, Neno, thibitisho la Kimaandiko lilipowashukia hao marabi na makuhani, walisema, “Huyu mtu ni ibilisi.”

229 Lakini wakati lilipomshukia maskini kahaba yule, kulifanyika nini? Upesi ilimulika ikawa Hai.

230 Hao marabi walisema, “Mtu huyu ana telepathia. Mtu huyu ni—ni—ni mpiga ramli. Hivyo ndivyo anavyoweza kuwaambia watu hao. Yeye ni mpiga ramli.”

231 Lakini mara Hilo lilipomgusa maskini kahaba huyo, katika hali hiyo! Kama lingalimuonya kahaba huyo, katika hali hiyo, linapaswa kufanya nini kwa kanisa la Kipentekoste linalodai kuwa na Roho Mtakatifu? Mnaona ninalomaanisha? Natumaini Hilo halitapita juu ya kichwa chako. Unaona? Unaona? Lilipaswa kufanya nini kwetu? Lakini mara lilipowamulika watu...

²³² Mara lilipommulika maskini mwanamke huyo, kamwe hakusema, “Wewe ni—wewe ni Beelizebuli.” Mwangalieni. Alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua. Tunajua. Tunamtazamia Mmoja kuja. Hatujawa na nabii kwa mamia ya miaka. Lakini tunajua ya kwamba Masihi atakuwa ni Nabii. Tunajua ya kwamba Yeye atatwambia mambo haya ajapo.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.”

²³³ Sasa, yeye alijua, Mtu aliyeweza kumwambia hayo, hakika angekuwa ni mwaminifu, kwa sababu alikuwa na Neno. Neno lilikuwa pamoja na Yeye, kwa kuwa Neno lilimjia nabii. Yeye alikuwa na fasiri ya kweli ya Hilo, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno. Basi mara Hilo lilipomgusa, yeye alivutiwa na hati ya mkataba mara moja. Alitaka kitega uchumi, upesi sana. Alitaka baadhi ya Maji hayo ambayo haikumbidi kuja kisimani kuchota. Basi mara alipoona Hilo, Hilo liliuwasha moto moyo wake.

²³⁴ Moja kwa moja akashuka mjini, kasema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hivi sivyo Masihi anavyopaswa kuwa?”

²³⁵ Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mjini walimwamini Yesu kwa sababu ya yale aliyomfanyia mwanamke huyo. Ushuhuda wake uliufanya mji huo kugeuka. Sasa, Yeye hakufanya miujiza yoyote. Alijua Filipo alikuwa anakuja kufanya hivyo.

²³⁶ Kwa hiyo, kama vile, Yohana hakuwa na miujiza yoyote, maana Yesu alikuwa amfuata.

²³⁷ Sasa, tunaona ya kwamba, ya kwamba waliwekeza katika hati hii ya mkataba, mara moja.

²³⁸ Hebu nichukue tu mwingine mmoja ama wawili, kama mtanisamehe kwa dakika moja, chache.

²³⁹ Nikodemo, siku moja, aliukubali ukweli. Mwajua, yeye alikuja usiku, kuwekeza, naye akapata Benki ilikuwa imefunguliwa. Sikuzote imefunguliwa. Akawaza, “Vema, Benki inafanya biashara mchana kutwa, kwa ajili ya uwekezaji huu, bali ninaamini nitaenda usiku.” Na, bali aliikuta Hiyo ikiwa imefunguliwa, tayari. Ndipo akasema, “Rabi, tunajua ya kwamba Wewe ni Mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Hakuna mtu angaliweza kufanya mambo haya ufanyayo, Mungu asipokuwa pamoja naye. Hilo haliwezekani kabisa.” Mnaona, alikubali pale, kwa ulimwengu wote wa kimadhehebu, ya kwamba walijua Hilo lilikuwa ni kweli. Lakini kwa upendeleo, na kiburi, na kupendwa sana na watu wa siku hizo, kama tu yule mtoto mdogo tajiri alivyofanya, kwa ajili ya sifa njema na hadhi ya umma, wala hawakutaka kuuacha ulimwengu.

²⁴⁰ Kama tu vile taifa hili lisivyotaka mtu mtauwa kule juu kutusahihisha. Hiyo ndiyo sababu tumeliwa na wadudu kwa

ukomunisti. Hawatamchukua mtu mtauwa. Watamchagua mtu ambaye anaweza kuwaacha waishi vyovyote watakavyo. Ni rahisi kwetu Wamarekani na sisi Wakristo kusema hivyo, bali tunaposhuka na . . .

²⁴¹ Sasa hebu tuzungumze na kulirejesha nyumbani mara moja. Ninyi wafuasi wa kanisa mnataka kitu kile kile. Mnataka mhubiri, ninyi wanawake, ambaye hatawahukumu kwa ajili ya vile mnavyoivalia na kuishi, mtu atakayewapapasa ninyi watu mgongoni na kuwaambia, kwamba, “Mnaweza kufanya *hili, lile*, na *linginelo*. Nanyi mnaweza kutenda kama ulimwengu na kuishi kama ulimwengu, na bado mdumishe maungamo yenu ya Kristo.” Mnayataka mambo hayo. Mnayapigia kura. Mtamwondoa kwa kura mtu mtauwa kutoka kwa jamii yenu, kumwingiza mtu kama huyo humo. Ndiyo shauku. Ndiyo roho ya taifa. Ndiyo roho ya siku za mwisho, mnataka kukiri na kushikilia maungamo yenu, “Mimi ni *hili*, mimi ni Mpentekoste, mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti,” na uendelee kushikilia hilo na kuishi vyovyote utakavyo.

²⁴² Yezebeli aliishikilia nchi vivyo hivyo, bali Mungu akawatumia mchungaji. Eliya alikuwa ndiye mchungaji wake. Loo, asingekubali hilo, bali yeye alikuwa, kwa vyovyote vile. Naam. Hakika.

²⁴³ “Mungu alikuwa anaweza kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Mungu haimlazimu kuja kupitia kwenye kundi lako wala kundi lingine lolote. Yeye ni Mungu. Hufanya yale Yeye atakayo kufanya, na Yeye atayafanya. Jambo moja Yeye asiloweza kufanya, hilo ni, kulikana Neno Lake Mwenyewe.

²⁴⁴ Kwa hiyo, Nikodemo alikuja, naye alitaka kuwekeza, basi akapata kile hasa alichokuwa akiomba. Yeye alikuwa ni mwaminifu. A—akakipata.

Hatuna budi kuharakisha.

²⁴⁵ Luka 24:49, kulikuwako na kundi la watu waliokuwa wamewekeza. Ndipo Yesu akawaambia, katika Luka 24:49, wale mia moja na ishirini, “Pandeni kule kwenye Siku ya Pentekoste huko juu, kisha mngoje hata mmevikwa uweza kutoka Juu. Nitawatumia riba ya huu pamoja nanyi, uwekezaji mliowekeza.”

²⁴⁶ Alikuwa amewapata. Alilichukua je tu kundi hilo? Alilichukua je kundi hilo dogo?

²⁴⁷ Siku moja wakati alipokuwa na huduma ya kuwaponya wagonjwa na kuonyesha Umasihi Wake, mbona, kila mtu, “Loo, ajabu, Rabi! Loo, njoo kwenye kanisa letu. Fanya mkutano hapa, Rabi. Tunakutaka Wewe *hapa*. Tunakutaka Wewe *hapa*.” Nalo kundi kubwa likianza kumfuata.

²⁴⁸ Lakini siku moja, ambapo, Mungu aliibadilisha huduma hiyo ndani Yake, kutoka kwa miujiza hadi kwa kufundisha Neno.

249 Hakika mnaweza kusoma katikati ya mistari. Ninyi si vipofu hivyo. Kama ndivyo ilivyo, unaweza kuweka penseli katikati ya macho yako na kuyang'oa macho yako, angalieni, angalieni, penseli ambayo ingeweza kuliandika Neno la Mungu.

250 Angalieni, mara Mungu alipoibadilisha huduma Yake kutoka kwa miujiza Yake. Miujiza Yake iliendelea, bali sio namna hiyo. Alianza kuwaambia Ukweli halisi wa Maandiko na mahali walipokuwa wamesimama. Umati huo ukamwacha. "Hili ni Neno gumu." Kulifanyika nini?

251 Wale sabini waliokuwa wakimfuata, aliokuwa amewachagua, wakaondoka, pia. Kasema, "Ni nani anayeweza kuelewa jambo kama Hili. Hilo ni kinyume na kila kitu tulichowahi kufundishwa." Kulifanyika nini?

252 Ndipo akawageukia wale kumi na wawili na kusema, "Nanyi mnataka kuondoka, pia?"

253 Hapo ndipo Petro aliposema lile neno zuri sana, "Bwana, twende wapi? Niambie jambo bora zaidi."

254 Loo, Mungu uturehemu! Unaweza kupata wapi kanuni yoyote ya imani iliyo bora kuliko Neno la Mungu? Ni wapi unapoweza kupata upendo wowote wenye kilindi zaidi kuliko upendo wa Yesu Kristo? Unaweza kupata wapi utoshelevu wowote wenye kilindi kuliko utoshelevu anaotoa Yesu Kristo?

255 Kitu kinachokufanya ufanye mambo ufanyayo, ni kwa sababu wewe ni... Inaonyesha utupu, mwanamke ambaye hupaka macho yake rangi ya samawati, na kukata nywele zake, na kujipaka rangi ya makucha. Na mwanamume atakayesimama na kumruhusu mke na watoto wake wafanye hivyo, inaonyesha kuna utupu mahali fulani. Huo unapaswa kujazwa na nguvu. Inapaswa kuwa ni Kristo humo ndani. Lakini inajishuhudia yenyewe.

256 Mtu ambaye angebadilisha dini, awalete waaminio kutoka kwenye kundi moja hadi lingine, inaonyesha kuna utupu mle. Anafanyia kazi dhehebu fulani badala ya Ufalme wa Mungu. Sijali wanakoenda, mradi tu wamezaliwa kwa Roho wa Mungu, wataishi maisha ya Kikristo. Utupu, matendo yanalishuhudia hilo.

257 Angalieni, walienda huko kwa ajili ya ujira. Naye Mungu alilipia kwenye uwekezaji huo waliokuwa wamefanya, kisha akawapa na zaidi.

258 Sasa, kama kundi hili la Kipentekoste linataka zaidi, wewe ishi vema na ufanye mema. Mungu ana mengi ya kulipia, nayo Benki imefunguliwa, mchana na usiku. Ila itawabidi kutokusema, "Vema, nadhani nitapanda huko mara moja."

259 Walipanda huko na kusema, "Vema, nadhani... Mnajua nini? Tumekuwa hapa juu kwa siku mbili. Mbona, nafikiri kama Yeye atafanya lolote..."

²⁶⁰ “Nimekuwa hapa madhabahuni, dakika ishirini. Kama Yeye atanipa Roho Mtakatifu, Yeye angenipa sasa.” Hayo ni, hayo ni mawazo yetu. Hapo ndipo tumefikia. Ule uaminifu . . .

²⁶¹ Loo, tunapenda kuwa kama watoto, tunapopigiwa filimbi, kucheza, na kadhalika. Lakini nashangaa juu ya jambo hilo.

²⁶² Ndipo, siku nane, siku tisa, vipi kama—vipi kama Mathayo angalisimama na kumwambia Si—Simoni, “Wajua nini? Yesu alitwambia tungoje hapa juu. Kimsingi tuko sawa. Tumengejea. Sasa, ninaamini tayari tumempokea Huyo. Mnaona? Ninaamini tulipokea. Hebu tuanze. *Wewe*, wewe kusanya kundi linaloitwa kwa jina lako. Na *wewe* kusanya kundi linaloitwa kwa jina lako. Nitawaambia, tutatoka twende tukaihubiri Injili sasa”? La, la. Hilo halikutenda kazi na Maandiko.

²⁶³ Isaya alisema, “Amri itakuwa juu ya amri, na kanuni juu ya kanuni; *hapa* patakuwapo na kidogo, na *pale* kidogo.” “Shikilia sana yaliyo mema.” “Kwa midomo ya watu wageni na lugha zingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo Raha. Huku ndiko kuburudika.” Wanajua Yoeli alikuwa ameahidi, “Katika siku za mwisho, nitamwaga,” Yoeli 2:28, “Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Kutakuwako na upako mkuu sana, hata nitaonyesha ishara katika mbingu juu na nchi chini, nguzo za moto na mvuke wa moshi.” Na, loo, jamani! Mnaona? Walingojea mpaka utambulisho wa Maandiko ukaja. Mnaona? Walikuwa wameuza yote. Walikuwa na uwekezaji wao. Walitaka ujira wa namna hiyo.

²⁶⁴ Leo hii, badala ya kanisa kufanya hivyo, tunajiuza kwa uanachama. “Tunaanza, tunawaleta ndani, chochote kile, kupata wengi kuliko Wamethodisti walio nao, ama Wabaptisti walio nao. Kupata wengi kuliko wa Umoja walio nao.” Nao wa Umoja zaidi ya wa utatu ama wa uwili, ama ni “wa-” wangapi mlio nao. Sijui mimi. Mnaona? Yote hayo, ni kitu gani? Ni lundo la malimwengu. Ni lundo la upuuzi. Mrudieni Mungu na Neno Lake lililothibitishwa. Amina.

²⁶⁵ Kijana tajiri Paulo wakati mmoja, huku amejaa thiolojia sana alivyoweza kuwa; kama yule kijana mtawala tajiri. Alikuwa akienda zake Dameski, naye akaona ya kwamba kulikuwako na Nuru iliyomulika mbele zake, Nguzo ya Moto, iliyoyapofusha macho yake. Ndipo akasema naye. Na Yeye akasema, “Sauli, ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo.” Basi wakati yeye . . . Ilihibitishwa kwake ya kwamba huyo alikuwa ni Yesu, aliyekuwa ni Mungu yeye yule wa Agano la Kale. Mnaona? Aliona Hiyo pale. Alikuwa akimfanya Huyo mtu mwingine, Beelizebuli fulani.

²⁶⁶ Lakini wakati alipoiona Nguzo hii ya Moto, alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ni Nguzo ile ile ya Moto ambayo alikuwa amefundishwa kwamba iliwaongoza Israeli. Na ilikuwa ndiyo

Hiyo hapo. Akasema, “U nani Wewe, Bwana?” Alimtambua kama Bwana kwa sababu ile Nguzo ya Moto ilikuwa pale.

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

²⁶⁷ Akafanya uwekezaji, pia. Alitaka Hilo. Kitu ambacho alikuwa amekichezea kwa muda mrefu sana, Hicho hapo moja kwa moja mbele yake. Akawekeza wakati alipothibitishiwa kikamilifu ya kwamba huyo alikuwa ni Yesu, na Yeye alikuwa ni Mungu. Alifanya lijulikane, “Bwana, ungetaka nifanye nini?”

²⁶⁸ Loo, ni uamuzi wa kijinga jinsi gani kijana huyu mtawala tajiri aliofanya! Sisi watu leo hii tunafikiri alifanya jambo baya mno. Yeye ni kama watu wa Laodikia siku hizi. Anataka umaarufu, sifa za watu, badala ya hati ya mkataba wa utumishi (*Hii* Ndiyo.) ambayo Mungu huwapa watu, waishi kwayo.

²⁶⁹ Yesu Kristo alikuwa ndiye Sura ya Mungu iliyodhihirishwa. Yeye alikuwa kile ambacho Mungu, kupitia nguvu Zake, alidhihirisha; mwili ambao uliitwa Mwana, kwa sababu Yeye alikuwa Mwanadamu. Na Yeye alitoka kwa Mungu. Na Yeye alikuwa amejitolea sana kwa Mungu, hata, hakuona kwamba Yeye na Mungu kuwa ni Mtu yule yule ni kitu cha kushikamana nacho. Nao walikuwa, kwa sababu Mungu alikuwa Neno, na Yeye alikuwa Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, na huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu.” Na hapo ambapo Mungu angeweza kulichukua Neno Lake, bila chochote, katizo lolote. Alikuwa daima akifanya yale Baba aliyotaka yafanywe. Na hapo Neno lingeweza kutenda kazi kupitia Yeye pale, hata Yeye na Baba walikuwa ni Mmoja. Hilo ndilo.

²⁷⁰ Ndipo basi akayachukua maisha hayo makamilifu, na dhambi zetu zote, na kuziweka juu ya maisha hayo makamilifu. Na Yeye alikufa ili kwamba sisi—sisi waasi tuweze. . . tuweze kufa kwa nafsi zetu, na kuzaliwa kutoka Juu, nalo Neno Lake lingeweza kutenda kazi za Mungu kupitia sisi.

²⁷¹ Loo, ni jambo la maana jinsi gani, kosa, ambalo kanisa limefanya, kama tu huyu jamaa kijana tajiri alilofanya. Utajiri wake uliongezeka. Loo, naam, alipata mali kama Laodikia, lakini a—akafanya kosa baya. Loo, jamani! Naye akawa mashuhuri sana na tajiri! Hebu tumfuatilie jamaa huyu kwa dakika chache tu sasa.

²⁷² Na, kwa kweli, nitaacha. Tazameni, angalieni. Yeye. . . [Ndugu mmoja anasema, “Lihubiri, Ndugu Branham!”—Mh.] Angalieni. Asante. Asante, ndugu.

²⁷³ Yeye, alijitajirisha. Sasa, watu wengi wanafikiri kwa sababu. . . Hapo ndipo ninapowasikia baadhi ya wafanyabiashara Wakristo, wakati mmoja, sikuzote wakishuhudia katika mikutano hii, jinsi Bwana alivyowafanikisha. Wakati mwingine hiyo kabisa ndiyo ukweli wa thibitisho lenyewe kwamba umeshindwa. Hiyo ni kweli. Jinsi kundi hili la Kipentekoste lilivyo tofauti na

vile lilivyokuwa katika siku hiyo! Wakati walipompokea Roho Mtakatifu, waliondolea mbali yote waliyokuwa nayo, wapate kuanza huduma. Naam. Basi, siku hizi, tunajaribu kusema tuna mamilioni, na yote kama hii hapa. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Sasa, hiyo ni kweli. Hakika ni kweli. Nasi tunajiita Pentekoste.

²⁷⁴ Nilisema hilo wakati mmoja, kwenye mmoja wa mikutano nilikowasikia baadhi ya hao watu wakishuhudia, Ndugu Demos na hao wengine walikuwako. Nikasema, “Ninyi watu, niko miongoni mweni kwa sababu ninawapenda, nami nafikiri mna kitu fulani. Ila niko hapa ndani kuwasaidia, kufanya yote niwezayo. Natumaini mnanielewa.” Nikasema, “Usiku wa leo, yote mliyofanya ilikuwa ni kusema mna Kadilaki ngapi, na kiasi gani m—mko tayari kuninii...” Nikasema, “Hao watu wana Kadilaki nyingi zaidi kuliko mtakazowahi kuwa nazo. Waambieni jinsi ya kukiondolea mbali kitu fulani walicho nacho, cha vitu hivi vya ulimwengu; wapate Kitu fulani moyoni mwao, Mungu Neno, kuthibitisha.” Mnaona?

²⁷⁵ Kulikuwako na maskini ndugu mzuri, wa Kipentekoste. Huenda ameketi hapa sasa. Sina chochote dhidi yake. Akasimama. Na wengi wa wafanyabiashara walioketi hapa wanajua hili ni kweli kabisa. Ndipo nikasema... Yeye akasema, “Lakini, Ndugu Branham, hapo ndipo kosa kubwa lilipofanywa.”

Nikasema, “Mungu alifanya kosa gani?”

²⁷⁶ Akasema, “Mbona, hao watu waliouza mali zao na—na kuzigawia maskini, kama Yesu alivyomwambia tajiri huyu kufanya, kuigawa miongoni mwa maskini, walifanya kosa. Kwa kuwa, mara mateso yalipoanza, hawakuwa na makazi ya kukimbilia.”

²⁷⁷ Nikasema, “Ndugu yangu, hivi unadai kuwa ni Mpentekoste, na kufikiria ya kwamba Roho Mtakatifu anaweza kufanya kosa? Neno la Mungu daima linabaki vile vile.”

Akasema, “Vema, hawakuwa na mahali popote pa kwenda.”

²⁷⁸ “Hiyo ndiyo hasa sababu ya Mungu kuwafanya wafanye hivyo. Ndipo wakaenda kutoka mahali hadi mahali, wakieneza injili. Hawakuwa na mahali pengine popote pa kwenda.” Mnaona? Ninajua. Lakini, leo hii, tunalichukulia vinginevyo kabisa.

²⁷⁹ Hebu tumtazame jamaa huyu kijana tajiri aliyefanya kosa hili la kijinga kama mfanyabiashara. Ninataka kuwaulizeni, ndugu. Hivi hilo si lilikuwa ni kosa baya sana kwa mfanyabiashara? [Ndugu mmoja anasema, “Naam.”—Mh.] Enyi kusanyiko, hivi hilo halikuwa ni kosa baya sana kwa mfanyabiashara? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Ni biashara gani kubwa zaidi a—angaliweza kufanikisha chochote kwayo, kuliko kuwa na Uzima wa Milele?

280 Ungeweza kutoa Kadilaki ngapi, mwishoni mwa safari yako? Demos Shakarian angalifanya nini hivi majuzi wakati moyo huo ulipoanza kurukaruka, naye alikuwa akizimia? Nawaulizeni. Wazieni hilo. Ufuasi wako wa kanisa, umashuhuri wako, utafanya nini? Itakuwaje kwako wakati ukiwa na vitu hivi vyote, kisha ikubidi kukutana na Mungu? Hakuna mifuko katika sanda. Unakutana na Mungu na nafsi yako. Na jinsi nafsi hiyo ilivyo, ilisababisha aina ya maisha uliyo. Na kama maisha hayo ndani yako yanalikana Neno hili, basi yaondolee mbali, na upate maisha yatakayodumu na hilo Neno na kumfanya Mungu aishi ndani yako. Kweli.

281 Kuna kasoro, kitu fulani hakitawafanya wanawake walainike vizuri. Sijali ni mara ngapi wanazungumza kwa lugha. Sijali ni mara ngapi wanafanya *hivi*. Hilo halimaanishi kitu. Tunda lako linanena kwa sauti kubwa kuliko sauti yako. Unaona? Hakika, linanena. Roho Mtakatifu ni unyenyekevu, mnyenyekevu.

282 Unasema, “Si lazima nifanye hivyo.” Ninajua si lazima. Wala, kondoo si lazima anyolewe, bali hutoa manyoya yake bure, ikiwa wewe ni kondoo. Sasa, mbuzi atasababisha ugomvi wa kila namna kulihusu. Kwa hiyo sasa mnaona mahali mnaposimama, wakati makasi ya Mungu yanapoanza kukunyoa. Sisemi kwamba . . .

283 Sisemi hilo kimzaha. Hapa si mahali pa mizaha. Hii ni mimbara. Hapa ni mahali ambapo hukumu inatolewa.

284 Sasa, kondoo atalala tu na kukuacha umnyoe, anapoteza haki zake.

285 Wewe ni Mmarekani. Unaweza kunyoa nywele zako. Unaweza. Unaweza. Unaweza kufanya lolote utakalo, Marekani. Unaweza kulewa, ulale mitaani. Na—na wewe unaweza kuwa kahaba. Unaweza kuishi na mwanamume, ama mwanamume aishi na mwanamke, awe kimada. Unaweza kuwa na wanne, watano, sita, saba, wanane, wote utakao. Haileti. . . Baadhi yao wana kumi na tano, ishirini. Mfano wako uko wapi? Haikubidi kufanya hivyo. Unasema, “Vema, kama mimi ni Mmarekani, hivi sina haki?” Naam, bwana. Hiyo ni kweli kabisa.

286 Lakini unapoteza haki zako kama wewe ni kondoo, wana-kondoo wa Mungu. Hiyo ni kweli. Unapoteza haki ulizo nazo.

287 Sasa, wazieni hili sasa wakati tukifunga. Naam. “Nimejitajirisha.” Naam, bwana. Sasa hebu tumfuate kidogo tu, na kisha tutafunga.

288 Tunaona, mahali pengine, ya kwamba kijana huyu tajiri alikuwa na mali nyingi sana mpaka hapana shaka alikuwa na kitu kama mlolongo wa Kadilaki.

289 Mwajua, wanasema, huko California sasa, “Usipokuwa na angalau Kadilaki tatu ama nne, na—na kumiliki mahali

pakubwa mno, wewe si wa kiroho.” Huenda ikawa ni “ukiroho wa ulimwengu.” Watu maskini; ninawajua wamishenari, wanaohubiri Injili, bila hata viatu miguuni mwao.

²⁹⁰ Nilipitia, hivi majuzi, nami nikaona mahali paliposema, “Makazi *haya* makubwa mno ya usoni ya *Fulani*.” Nikaenda *hapa*, “Makazi *haya* makubwa mno ya baadaye ya *Fulani*.”

Ndipo nikasema, “Mungu, na mimi je?”

Yeye akasema, “Tazama juu.” Kweli.

²⁹¹ Wakati kodi ya mapato iliponiwekea mzungu hivi majuzi, na kwa ajili ya hundi ambazo watu walikuwa wametia sahihi kwenye mkutano, kuulipia mkutano. Kodi ya mapato ilirudi nyuma miaka kumi na mitano, na—na kunifanya niwalipe dola elfu arobaini. Ilinibidi nipate watu wa kunisimamia na kadhalika. Nao wameketi moja wa moja kwenye jengo hili sasa, kutia sahihi tikiti, kwamba ningeweza kuilipia kwa dola elfu nne kwa mwaka, ama nifikishwe mbele ya mahakama. Nikasema, “Si—sina deni ya hiyo. Haya hapa makaratasi yangu, ya kodi yangu ya mapato.”

²⁹² Kasema, “Naam. Lakini wakati hao watu walipotia sahihi hundi hiyo, wao... Ulijitambulisha mwenyewe wakati ulipoitia sahihi. Ilikuwa ni yako. Ndipo ukaitoa, kulipia gharama ya mkutano.” Mnaona?

²⁹³ Hiyo ni haki? La, bwana. Hakuna haki. Nilifikiria vibaya sana juu yake. Basi, nikaangalia katika Biblia, na kuona ya kwamba kila mtu aliyepata kuwa na ofisi ya kiroho, katika Biblia, alihusishwa na serikali. Serikali ilimnasa, maana ni kiti cha ibilisi. Rejea nyuma, Musa, Yereima, Danieli, manabii wote, hata kwa Yesu Kristo, alikufa chini ya adhabu ya kifo ya serikali. Hawawezi kuwashika kwa uadilifu na chochote kingine, kwa hiyo ibilisi, kiti chake kikuu, huliweka moja kwa moja na serikali. Hiyo ni kweli kabisa. Naam.

²⁹⁴ Mtu huyu tajiri alikuwa ametajirika zaidi, jamani, ambapo mtu angeweza...

²⁹⁵ Dola elfu arobaini, kile hilo lilichomaanisha kwa mtu, kulipa namna hiyo. Nina miaka kumi ya kuilipa, kwa dola elfu nne kila mwaka. Ninapata dola mia moja kwa juma. Ningalikuwa nazo. Hiyo ni kweli kabisa. Sijihurumii. Ninawaambia jambo fulani, kile mimi... Mfano tu ama kitu fulani, ili mweze kuelewa.

²⁹⁶ Ningalikuwa nazo, kama ningalichukua pesa watu walizokuwa wamenipa. Ningekuwa zaidi ya milionea. Ningalikuwa na milolongo, ya majengo, isingewalazimu kukodisha hili. Ningesema, “Njoni, lichukueni.” Mnaona?

²⁹⁷ Lakini, jamani, nimejaribu kuwazia hilo, kumfanya Yesu Kristo Mfano wangu. Angaliweza kuwaumba samaki. Angaliweza kuumba pesa. Angeweza kufanya divai kutokana na maji. Angeweza kulisha, kwa—kwa maelfu, kwa samaki

wawili na—na mkate mmoja ama miwili. Lakini, hata hivyo, Yeye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Yeye alikuwa ni Mfano wetu. Si kitu cha kung’aa, bali kitu ambacho humeka, Injili.

²⁹⁸ Hapo tunamwona tajiri huyu, mpaka akawa na vitu vingi sana, hata maghala yake yote yakajaa kabisa, na kila kitu. Alisema. “Sasa, mnaona, kama ningaliwafuata hao walokole, mnaona mahali ningalikuwa? Unaona? Lakini sasa nimeishi katika heba, wanawake wote wamenizunguka, nami nina haya yote *ambayo* ninataka, na nina *ninii* yote. Nina uhusiano mzuri na makuhani wote, marabi. Wote hunipapasa mgongoni, na kusema, ‘Ndugu Jones, tuna furaha sana kukuona.’”

Natumaini hakuna Ndugu Jones hapa asubuhi ya leo.

²⁹⁹ Lakini, kumpapasa mgongoni, na kusema, “Ndugu, tuna furaha sana kuwa nawe!” “Loo, ninyi watu wote, hebu kidogo tu. Sasa, ninataka kuwaonyesha, huyo hapo Dk. Levi Levinski Jones ameketi,” yeyote yule, “ameketi hapa. Ni mmoja wa wasaidizi. Yeye hutujengea kanisa. Hufanya *hiki, kile*, ama *kinginecho*.” Hum. Hakika. Sasa, hiyo ndiyo hali yake pale. Anang’ara kama Hollywood. Labda wasichana waimbaji kwenye vilabu na kadhalika waliomzunguka walikuwa wazuri sana. Naye alikuwa na yote aliyotaka ya anasa za ulimwengu huu. Hiyo ni kweli.

³⁰⁰ Na hapo palikuwa na maskini wa roho, amelala hapo nje, akiomba makombo machache. Mathayo 5, ilisema, “Heri walio maskini wa roho.” Tunamwona Lazaro huko nje akiwa hana kitu. Mnawazia nini juu yake? Alifagia makombo machache, mara kwa mara, kumlisha. Nashangaa. Naam.

³⁰¹ Lakini malipo yake hatimaye yakaja. Naam, akapata malipo yake. Nawe utapata, pia, nami vile vile na kila mwanadamu. Ninafunga. Malipo yake yalikuja. Alipata nini? Ibada kubwa ya mazishi. Ninaweza kuwazia, kapera fulani mwenye ukosi uliopinduliwa, “Baba Mtakatifu.”

³⁰² Ninyi Wapentekoste mna shida gani, kuwaita jamaa hawa hapa “Baba”? Ninaliona katika gazeti lenu. Huyu mhariri ana shida gani, hata hivyo? Nilifikiri mlikuwa Pentekoste. Kusimama hapa na kusema, “Baba Mtakatifu *Fulani-wa-fulani*,” mkisema hivyo.

³⁰³ Biblia ilisema, “Msimwite mtu yeyote Baba,” namna hiyo. “Mnaye Baba mmoja, huyo ni Yesu Kristo.”

³⁰⁴ Kuna shida gani? Mnaona kile ninachowaambia? Ninyi ni, ninyi ni. . . Magugu tayari yamewapata. Afadhali mkikatilie mbali kitu hicho, sasa hivi.

³⁰⁵ Heri msikilize yale ninayowaambia. Huenda msipende kufanya hivyo, kwa sababu mimi ni “mjinga.” Lakini mimi si mjinga hivyo, labda, kama mnavyodhania nilivyo. Mnaona? Huenda nikawa. Labda inambidi Mungu kuchukua kitu kijinga.

Mnaona? Kwa neema Yake, ninaliona likija. Ninaona maandishi ya mkono juu ya ukuta. Jinyosheni, la sivyo mtatolewa nje. Hilo ni neno kubwa kwa mtu kusema. Sisemi hilo kwa nafsi yangu. Nimevuviwa kusema hili, la sivyo nisingekuwa ninalisema, kadiri ninavyowapenda wanaume na wanawake, kadiri ninavyowapenda.

³⁰⁶ Hebu niwaambie jambo fulani. Katika Yohana wa Kwanza 4:17, tunaona, ya kwamba, kukemea kwa nguvu ni upendo tu ukijitokeza wenyewe kwa ajili ya Hukumu. Hiyo ni kweli. Ni kwa sababu tu ya upendo.

³⁰⁷ Kama ukimwona mtoto wako mdogo huko nje mtaani naye anaenda kuuawa, hivi ungesema, “Vema, Kadogoo. Riki, kipenzi, wewe kaa papo hapo. Unajiburudisha”? Ungekuwa mfano duni wa mama, ama baba hafifu. Ungemwingiza mle ndani na, kama akilirudia tena, ungemgeuza mkononi mwako na kumpa anachopaswa kupata. Hakika. Ungemcharaza sana hivi—hivi kwamba angeogopa kutoka nje tena.

³⁰⁸ Hivyo ndivyo Mungu anavyowafanya Wake. Husemi hilo kuwa mbaya. Unalisema kwa ajili ya upendo. Watu wamechanganyikiwa na mambo yote, wakifikiri kwamba upendo ni kitu kama kitoto cha mbwa. Upendo ni mnyofu. Mungu ni upendo. Mungu hukemea na kurudi kwa sababu ya upendo. Natumaini hilo linazama kwa kilindi kabisa kama ninavyolitaka lizame, mnaona, kwamba ni—ni upendo unaosahihisha. Ni upendo unaosahihisha. Na upendo halisi utastahimili masahihisho. Lakini mpapaso wa kitoto cha mbwa mgongoni, na “Dk. *Fulani-wa-fulani*, Askofu *Fulani-wa-fulani*,” wakati mwingine humfanya Roho Mtakatifu kulia moyoni mwako. Hiyo ni kweli.

³⁰⁹ Ibada kubwa ya kimadhehebu, mashemasi wote wakaja huko, na viongozi wote wakuu. Nao wakafanya ibada kubwa. Na, loo, Shirika la Wafanyabiashara wa mjini walikuja, na kusema, “Ndugu yetu wa thamani aliyejenga *hili*, na ndugu yetu wa thamani aliyejenga hilo, yuko huko ng’ambo kabisa katika mikono ya Utukufu, akiwa tu na wakati mzuri.”

³¹⁰ Nayo Biblia ilisema, “Akainua macho yake kuzimuni.” Naye akamwona yule mtu maskini wa roho, maskini katika roho, huko ng’ambo pamoja na urithi wake kutoka kwenye uwekezaji wake. Aliwekeza vibaya, mtu huyu. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Alimwona mmiliki wa hati ya mkataba unaoukubali Uzima wa Milele, naye alikuwa huko ng’ambo Mbinguni. Na alijua alimpa tu makombo, ku—kumsaidia, si mambo aliyopaswa kufanya. Hakuwa ameyatoa maisha yake juu ya nafasi ambayo Kristo alimpa.

³¹¹ Wasemaji hodari wakaja, na kusema, “Ndugu yetu wa thamani, yeye ni *hivi-na-hivi*.” Mwanadamu anaweza kusema jambo moja, bali Mungu anasema jambo lingine. Mnaona? Nasi

tunaona ya kwamba maisha yake yasingelingana, yasingetoa kile Neno la Mungu lilichohitaji. Sasa nawatakeni muwazie juu ya yenu, ninapowazia juu ya yangu. Mnaona? Wasemaji wake hodari, watu mashuhuri walisimama kwenye mazishi yake. Jinsi ilivyokuwa tofauti na mazishi ya Ibrahimu!

³¹² Ibrahimu alikuwa ameacha utajiri wote, hata mguu wake ukiwa juu ya kiti cha enzi kuwa Farao wa Misri. Naye akauacha, akihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko makanisa yote na madoido ya Misri. Alifanya nini? Wakati Ibrahimu alipokufa, kulifanyika nini? Ninamaanisha Musa, badala ya Ibrahimu. Samahani. Musa, wakati alipokufa, yeye, mnajua alikuwa na wabeba jeneza wa aina gani? Malaika. Kwa nini? Mwanadamu asingeweza kumbeba kumpeleka alikokuwa akienda. Ilibidi awe na Malaika, kumbeba wampeleke alikokuwa anaenda. Kwa nini? Alikuwa ameyaacha madoido ya ulimwengu, na kuchukua shutuma la Kristo.

³¹³ Ninyi, asubuhi ya leo, ndugu zangu, mko katika hali hiyo? Hiyo ndiyo hali yako ya kisasa sasa, hali yako ya sasa? Hivi inakukuta ukiwa tayari kulipokea?

³¹⁴ Ninyi dada, hali yenu ya sasa, mtageuka upande Huu na kusema, “Ee, Ndugu Branham, na—nampenda, ila kidogo amerukwa na akili”?

³¹⁵ Labda niko hivyo. Kama sina kichwa kizuri, ninataka kuwa hivyo, kusudi niweze kuwa katika kichwa Chake. “Nia iliyokuwamo katika Kristo na iwe ndani yenu, na msem Kweli tupu.” Hakika. Sasa, kumbukeni, mfuateni Kristo.

³¹⁶ Tunaona ya kwamba, Musa, yeye alikuwa na Wabeba jeneza waliopaswa kumpeleka juu. Mwanadamu asingeweza kufanya hivyo.

³¹⁷ Lakini tajiri huyu labda alikuwa na watu mashuhuri wa mjini, waliobeba jeneza lake, bali katika kuzimu aliinua macho yake. Lakini kwa nini? Uwekezaji wake katika ninii. . .

³¹⁸ Sasa, alikuwa ni mfuasi wa kanisa. Mnasema hakuwa. Yeye alikuwa. Biblia ilisema alikuwa. Alimwita Ibrahimu “baba,” mnaona. “Baba Ibrahimu,” mnaona, “mtume Lazaro.”

³¹⁹ Lakini, yeye alikuwa mfuasi wa kanisa aliyekiri, bali hakutaka uwekezaji wo—wowote katika Yesu Kristo, kwa hiyo mnaona mahali alipoyainua macho yake: katika kuzimu.

³²⁰ Ndipo, akamwona ombaomba huyu mbali sana kifufuni mwa Ibrahimu, ndipo yeye akawa ombaomba.

³²¹ Utaombaomba, wakati mmoja. Unajua hilo? Utaombaomba, wakati mmoja. Kwa hiyo, kama wewe huko sawa na Mungu, anza kuomba sasa hivi, upate kuondoa ugumu wote kutoka kwako, ulimwengu wote kutoka kwako. Omba rehema. Usipoomba,

utakuta hali yako mahali pale pale jamaa huyu kijana tajiri alipojikuta, wakati alipopewa nafasi.

³²² Kama vile, imewasilishwa kwenu kwa Neno la Mungu lililothibitishwa likifanyika binafsi. Amina. Najisikia sasa kama vile mpentekoste anavyopaswa kujisikia. Neno, Kweli, utafanya nini na Hiyo? Utafanya nini, kuikwepa Hiyo, na kwenda huko nje na kufanya jambo lingine, kutoka nje na kula chakula chako cha kutwa? Inapaswa kusababisha m—mkutano wa maombi. Inapaswa kusababisha kufunga. Inapaswa kusababisha. . .

³²³ Basi unaweza kufanya hivyo namna gani wakati hakuna kitu pale cha kufanyia? Hakuna shauku, hakuna uaminifu! Hebu mtu aje na kulikanusha Hilo, kwa Neno. Mungu huthibitisha Neno Lake. Aliahidi ya kwamba Yeye angefanya hivyo. Sikuzote alifanya hivyo.

³²⁴ Kwa hiyo, mnaona, yeye akawa ombaomba, hata hivyo. Wakati mwingine inatulazimu kuomba. Usifanye kosa lako kama yeye alivyofanya. Wekeza asubuhi hii katika Yesu Kristo.

³²⁵ Nitamchukua tajiri mwingine mmoja, mmoja tu, kwa kama dakika moja.

³²⁶ Ndiyo kwanza nimalize *Baraza la Nikea, Lililotangulia Nikea, Baraza Lililoifuata Nikea*, na *Wazee wa Nikea*, vyote, kuona mahali kanisa, kuona tu ambapo lilifanya kosa lake.

³²⁷ Niliyafikia maandishi ya Mtakatifu Martin, Tours, Mfaransa. Nami ninaona ya kwamba alizaliwa katika nyumba tajiri. Baba yake alikuwa ni mwanajeshi mashuhuri. Na huko Ufaransa, siku hizo, ilikuwa ni amri kwamba mwana anapaswa kufanya aliyofanya baba yake.

³²⁸ Nafikiri hilo lingali ni jambo jema katika njia ya Kikristo. Ikiwa Huyu ni Baba yako, unafuata nyayo Zake.

³²⁹ Sasa tunaona ya kwamba Martin alikuwa—alikuwa awe a—askari. Naye alikuwa, wito maishani mwake, wa Mungu. Naye ni mnyenyekevu, wanajua. Kila askari alikuwa na m—mtu aliyepaswa kupiga buti zake rangi, na—na kumshugulikia, kumfanya nadhifu, kwa sababu yeye alikuwa ni mfano kwa taifa, mbele za watu. Nao walisema, “Badala ya—ya mtumishi wa Martin, labda mvulana mweusi aliyekuwa azipige rangi buti zake, yeye alizipiga rangi buti za mvulana huyo mweusi.” Na, hata hivyo, hata hakuwa Mkristo bado. Alikuwa ni kafiri, bali mbegu hiyo iliyokusudiwa tangu zamani ilikaa mle.

³³⁰ Kama tu ilivyofanya katika maskini mwanamke yule, wakati alipouona ule mwujiza, kwamba Yesu angeweza kumwambia shida yake ilikuwa wapi. Ilimulika namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] Ikawa Hai. Mwana akaiangazia.

³³¹ Na wewe—wewe huwezi kuuzuia uhai chini wakati jua linapoiangazia mbegu. Mbegu inaweza kukaa pale pasipo na

uhai ndani yake, itakaa tu pale. Lakini ikiwa ina uhai ndani yake, utatokea wakati jua likiiangazia.

³³² Naye Martin, hata hivyo, wito huo maishani mwake, na yeye—yeye alitaka kuninii—alitaka kumfanyia Mungu jambo fulani, na hakujua la kufanya. Naye akasema... Siku moja alisimama karibu na lango, wakati watu wakiingia mjini, majira ya baridi kwelikweli.

³³³ Kama tuliyo nayo huko Mashariki sasa. Ndio kwanza nisikie kutoka nyumbani, ilikuwa ni ishirini chini ya sufuri, na huko Indiana. Hiyo karibu ni rekodi. Nadhani ni rekodi.

³³⁴ Baridi sana, nao watu maskini wamekaa huko nje, bila chakula, na wanaganda hata kufa. Basi Martin, Mtakatifu Martin, akaja kupitia langoni, na—na hapo akaona maskini ombaomba amelala pale. Basi maskini jamaa huyo mzee alikuwa na matambara. Alikuwa anaganda. Ndipo Martin akasimama.

³³⁵ Ndipo watu wakapita hapo, matajiri sana. Naye akasema, “Tafadhali, bwana. Nafa. Hivi huwezi, huwezi kunipa kitu? Ninaganda. Si—siwezi kumaliza usiku huu. Tafadhali usiniache nife.” Nao wakapita tu, kwa sababu hakuwa kitu ila ombaomba.

³³⁶ Martin akasimama na kuangalia hali hiyo. Yeye alikuwa ametoa kila kitu alichokuwa nacho. A—akachukua... Alikuwa na koti moja. Ilikuwa ni shali, kitu kama hicho. Ilipitia mabegani mwake; askari walikuwa nayo siku hizo. Naye alikuwa na moja kubwa, ndefu, kama blanketi mabegani mwake. Basi akasimama. Alijua ataganda, pia, usiku huo, kama hakuwa nayo. Kwa hiyo akauchukua upanga wake na kuikata, nusu, vipande viwili. Akaenda pale akamfunika nayo maskini yule ombaomba, akachukua ile nusu nyingine akajizungushia.

³³⁷ Aliposhuka barabarani, kwa kufanya mbinu kama hiyo, walimcheka, kasema, “Ni askari anayeonekana wa kuchekesha jinsi gani!”

³³⁸ Hapana shaka, leo hii, ukisimama kwenye Neno, ukiitetea Kweli, ulimwengu wa kimadhehebu utasema, “Unaonekana kama kitu cha kuchekesha. Ulitoka kwenye kanuni gani ya imani? Ziko wapi hati za utambulisho wako?” Kweli. Unapojaribu kufanya yaliyo sahihi, ukijaribu kufanya yaliyo sahihi kwa Neno la Mungu.

³³⁹ Usiku huo, wakati Martin alipokuwa amelala, aliamshwa, katika usingizi wake. Aliangalia. Huyo hapo Yesu amesimama, amesimama chumbani, naye alikuwa amefunikwa kipande kile cha vazi ambacho alimfunikia yule mzee. Mnaona?

³⁴⁰ Aliwekeza. Akapata wito wake pale. Naye alikuwa ndiye mjumbe wa wakati huo. Alilirejesha kanisa kwenye ka—kanuni za kipentekoste. Mtu mashuhuri!

³⁴¹ Si muda mrefu uliopita, nikiangalia orodha ya Wafia imani, kadi yake, niliomba kadi ya Mtakatifu Martin. Rafiki

huyu Mkatoliki akasema, “Mbona, yeye haku—hakufanywa mtakatifu.”

³⁴² Huenda nisifanywe mtakatifu, na kanisa katoliki la Kirumi, bali alikuwa kwenye Kitabu cha Mungu. Yeye alilirejesha kanisa kwenye kanuni za Injili, kurudi kwenye ubatizo asili wa Roho Mtakatifu, kurudi kwenye Uzima halisi wa Mungu. Kwa nini? Alifanya yaliyokuwa mema. Aliwekeza kutoka kwenye utajiri wake, kutoka kwenye utajiri wake wa hazina za duniani na utajiri wa—wa yale aliyokuwa, ndipo akauza yote na kuwa mwekezaji halisi katika Yesu Kristo. Na tulichukue jambo lilo hilo asubuhi ya leo.

³⁴³ Asanteni, kwa usikivu wenu. Samahani kwa kuwaweka muda huu wote.

³⁴⁴ Sijui, huenda huu ukawa ndio wangu wa mwisho. Lakini, ukifika, wakati wangu hatimaye ukifika, sina budi kukutana nao siku moja.

³⁴⁵ Mtakapoicheza kanda hiyo, mtaelewa. Sijui litakalotukia.

³⁴⁶ Lakini kutoka moyoni mwangu, kama mpenda Pentekoste, ni kwa nini nipo hapa pamoja nanyi? Baadhi yenu ninyi ndugu wa kimadhehebu mnasema, “Anayachukia madhehebu yetu.” Siyachukii. Ninauchukia mfumo unaowakokota kuwaingiza ulimwengu.

³⁴⁷ Kama nilidhani Methodisti ilikuwa sahihi, ningekuwa pamoja nao. Kama niliwazia Baptisti ilikuwa sahihi... Nimetoka kwao, kuwa pamoja nanyi. Watu wangu ni Wakatoliki. Kama ningaliwazia hiyo ilikuwa sahihi, ningekuwa pamoja nao. Niliwaacha, kuja kwenu, kwa sababu nafikiri ninyi ndio kitu cha karibu sana papo hapo kilichopo. Ninaamini hilo. Kama sivyo, ningekuwa nikiweka jitihada zangu mahali pengine.

³⁴⁸ Mnajua sijawahi kuwaomba hata senti moja. Kamwe sijawaomba, hata nisingechukua kile mnachonipa. Si kwa ajili ya pesa.

³⁴⁹ Ninawatakeni mkumbuke, kama alivyosema Samweli, wakati walipotaka mfalme juu yao. Alisema, “Hiyo ni kama ulimwengu. Msifanye hivyo. Ninyi watu mna Mungu mmoja, Mfalme mmoja. Dumuni na Yeye.” Ndipo wanalitaka, kwa vyovyote vile. Walitaka kuonekana kama ulimwengu mwingine wote. Ni picha ya jinsi gani ya kanisa la Kipentekoste!

³⁵⁰ Samweli alisimama pale asubuhi hiyo, naye akasema, “Angalieni. Hivi nimewahi kuchukua chochote kutoka kwenu, pesa zenu?”

“La, hujafanya hivyo.”

³⁵¹ “Nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lile lililotimia?”

352 Nao Israeli, katika sauti moja, wakasema, “Ni kweli. Hujawahi kunena katika Jina la Bwana ila lile lililotimia.”

“Basi,” kasema, “nisikieni. Mungu ndiye mfalme wenu.”

“Lakini tunataka mfalme, kwa vyovyote vile.”

353 Na hilo mtafanya. Na tuombe. Nafikiri nimeenda umbali tu ninavyojua jinsi ya kuenda.

354 Baba wa Mbinguni, sisi ni... Roho iliyo ndani ya watu huwafanya watafute kitu fulani. Ni kama tu Kayafa alivyosema, “Si ni vema kwamba Mtu mmoja afe, kuliko ulimwengu mzima kuangamia, taifa zima kuangamia, hasa?” Nayo Biblia ilisema yeye alitabiri, akiwa ni kuhani mkuu. Roho alikuwa na haki ya kungusa. Lakini jinsi alivyokuwa amepotoka kwa mbali, kumsulubisha Mungu yule hasa ambaye alidai kwamba anamtumikia.

355 Jinsi walivyokariri hekaluni, “Mungu wangu, mbona Wewe umeniacha?” Na Mungu yeye yule waliyekuwa wakinena habari zake, alikuwa akiyakariri msalabani, katika utimilifu.

356 Bwana, hakuna njia niiuayo ya kufungua macho ya watu hawa. Siwezi kuwaomba wanisamehe kwa kuwakatakata. Ninawezaje kufanya hivyo, na kudumu mwaminifu Kwako? Wala sisemi hili, wapate kunisikia. Nikifanya hivyo, ni—ningeenda kwenye madhabahu haya, nikatubu, kama mnafiki. Lakini sasa, kwa miaka, Bwana...

357 Hebu waone ya kwamba kwa sababu kwamba—kwamba wanayo miguso ya Roho hapa, hata zaidi ya ndugu zao, na hilo ndilo linalowafanya watafute kitu fulani. Lakini, Bwana, Wewe huwezi kulijenga Kanisa Lako juu ya kitu kama hicho, wakati wanaheshimiana, mmoja kwa mwingine. “Mungu hatashiriki Utukufu Wake na mtu yeyote.” Jalia waachilie mambo ya ulimwengu.

358 Mungu, bariki kundi hili la Wafanyabiashara. Umewafanya o—oasisi kwa ajili ya huduma yangu. Ninaamini uliliinua jinsi hiyo. Hata katika mikato yote migumu, hata hivyo ulimzuia yeyote wao kuniwazia uovu. Wao hunialika nirudi tena moja kwa moja. Ninajua ni njia Yako ya kuwafikia watu, Bwana. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utayaheshimu yale niliyosema.

359 Na iwapo wakati wangu umekwisha, Bwana, jalia niondoke kwa amani. Jalia niende, pasipo kuishikilia damu ya mtu yeyote mikononi mwangu, wala kanisa, wala kanuni ya imani ya kimadhehebu, wala chochote kile, bali pamoja na Damu ya Yesu Kristo. Tujalie, Bwana.

360 Ndugu zangu wa kimadheheu huko nje, Bwana, wengi wao, kuna wazuri, baadhi ya ndugu wazuri sana niliowahi kukutana nao, katika hao wote, kila mahali. Basi ni kwa nini wanafanya hivyo, Bwana? Wakati, Wewe utageuka moja kwa moja na kuthibitisha Neno hilo kuwa ni Kweli, na kuonyesha ya kwamba,

ishara ile ile iliyopaswa kutukia katika siku za mwisho, ya ufufuo, kwamba Kristo yupo hapa. Na si mtu fulani. Kwamba, ni Roho Mtakatifu Mwenyewe.

³⁶¹ Mungu, ninamkemea huyo ibilisi. Ninazikemea nguvu za mtindo, na nguvu za ulimwengu, ambazo zinayapofusha macho ya Kanisa Lako, Bwana. Ninaomba ya kwamba ataondolewa kwao, hata watakugeukia Wewe kwa moyo wote, na kukutumikia Wewe siku zote za maisha yao.

³⁶² Tusamehe, Ee Bwana. Ninasimama kama Isaya asubuhi ile, aliyekuwa ameliona lile ono. Alisema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na miongoni mwa watu waovu wenye midomo michafu.” Bwana, jalia yule Malaika aje tena. Pia jalia Yeye alete Moto kutoka madhabahuni, na kugusa midomo ya kila mmoja wetu, Bwana, ili tuseme yaliyo Kweli pekee, na yaliyo Neno, na yaliyo sahihi; tupate kuiita siku hii yenye dhambi ya—ya Umarekani uliochanganyishwa na ulimwengu, ukaingizwa kanisani, irudi kwenye toba.

³⁶³ Mungu, tuliliombea jambo hilo, kwa miaka. Na wakati linapotumwa kwetu, linakuja kwa njia nyenyekevu. Kama nilivyosema, waliomba wapate a—askari wa vita, nao wakapata mtoto mchanga. Lakini ndiye uliyewatumia, wala wasingempokea. Mungu, jalia watu wasifanye kosa tena, kuona Hilo. Si kanuni mpya ya imani, dhehebu jipya, bali kurudi kwenye Neno, kumrudia Mungu, Neno lililothibitishwa. Tujalie, Baba.

³⁶⁴ Mbariki Ndugu yetu Shakarian, ninahisi roho yake ikiingia kutoka nyuma yangu, tunajua kwamba yeye ni mnyonge, tunajua ya kwamba Shetani anaufuatilia uhai wake kwa dhati sasa. Mungu, ninayadai maisha yake, mpaka Wewe utakapomaliza na siku hii—hii ya mwisho hapa. Tusaidie. Jalia tuombe ombi hili la imani; maskini mke wake mpendwa.

³⁶⁵ Ninawaombea hawa wafanyabiashara, kwa ajili ya hawa wenye mamlaka, na hawa—hawa wahudumu. Ee Mungu, tafadhali, naomba katika Jina la Yesu! Nisaidie, Mungu. Nisaidie. Sijui niseme nini tena. Moyo wangu unawaka moto. Nafsi yangu inaona shauku. Jalia waje, Bwana, kwa utamu, sio kwa kitu nilichosema, bali jalia warudi kwenye Neno, Bwana, na waone, na wakae pale mpaka waone likitukia. Lijalie.

³⁶⁶ Pia, Baba, nimeitawanya Mbegu. Ninajua, wakati Hiyo inapoanguka kwenye udongo huo uliokusudiwa tangu zamani, Hiyo itawaka na kuangaza, ikimeka kwa ajili ya Utukufu wa Mungu. Tusaidie, Baba. Tunayakabidhi haya Kwako sasa, katika Jina la Bwana Yesu.

³⁶⁷ Huku tumeviinamisha vichwa vyetu, kungekuwako na wengine hapa asubuhi ya leo, wangesema, “Ndugu Branham, kweli ndani ya moyo wangu ninaamini hiyo ni kweli, na mimi—

mimi nataka kurudi. Na—nataka kitega uchumi asubuhi ya leo. Sio—sio tena katika ninii . . . Nitakaa kanisani mwangu”?

³⁶⁸ Usiondoke kanisani mwako. La, bwana. Wewe kaa moja kwa moja kanisani mwako, popote ulipo, na umpende mchungaji wako, na uwapende wafuasi wote, na kila kitu kingine. Wapende hao. Lakini, loo, kaa humo, sio kung’aa kwa kitu fulani cha ulimwengu, sio kuweka kitu tofauti, bali kumeka kwa Utukufu wa Mungu, katika unyenyekevu, kuwa tayari kuchukua shutuma kama wakikuwa wa mtindo wa kale. Nawe ni . . .

³⁶⁹ Katika kanisa mashuhuri, hivi majuzi, moja ya madhehebu makubwa sana ya Pentekoste; mtu mmoja, mhudumu, alisimama. Basi mama mmoja alikuwa na nywele ndefu, nayo ilisokotwa nyuma yake. Kasema, “Puto lako linapaswa kuondolewa upepo.” Kasema, “Wewe ni tofauti na hao wengine.” Maskini hali hiyo, iliyorudi nyuma! Hum. Ni wakati wa jinsi gani!

³⁷⁰ Loo, utalikubali? Inua mkono wako, useme, “Mimi, mimi nitakubali. Nitaamini. Mungu, ninataka kuwekeza asubuhi ya leo. Ninataka kusalimisha maisha yangu. Ninataka kuwekeza. Nimekuwa . . . Nimepewa nafasi. Ndugu Branham, ninajua ya kwamba—ya kwamba Mungu hana budi kusema nawe, la sivyo usingefanya mambo haya. Ninajua haya yanatoka kwa Mungu. Ninataka kuwekeza, nami nitasimama kwa miguu yangu sasa hivi na kusema, ‘Nataka kuwekeza. Ninayaweka maisha yangu wakfu upya, sasa hivi, kwa Yesu Kristo.’”

³⁷¹ Simameni kwa miguu yenu, kila mahali, na kusema, “Ninayawekeza yangu.” Baba wa Mbinguni, hebu tumwinulie mikono yetu sasa.

³⁷² Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, tunajiweka wakfu. Sijui kile litakalomaanisha. Baadhi yao kweli wanalimaanisha, nadhani, Bwana. Baadhi yao wanasimama tu. Baadhi wanasimama maana wengine wanasimama. Baadhi yao wanasimama kwa sababu Wewe unasema nao. Wengine wamesikia Neno la Mungu. Mungu, siwezi kuligawa. Lakini ninaomba ya kwamba Wewe utaligawa, Bwana, sasa. Na kumtuma Roho Mtakatifu, na ibada kuu ya kujiweka wakfu kwa Mungu.

³⁷³ Sasa inueni tu mikono yenu na mioyo yenu. Msijali kuhusu mlo wa kutwa. Huo unaleta tofauti gani? Mmepata . . . Msijali kuhusu huo.

³⁷⁴ Ni, sasa hivi, usiku wa manane. Sayansi inasema, “Ni dakika tatu ifike usiku wa manane.” Lakini huenda hii ikawa ndiyo saa yako ya usiku wa manane. Kabisa, ni saa sita, juu ya alama. Sikujua hilo. Na hii huenda ikawa ndiyo saa sita, mpigo wa usiku wa manane kwa baadhi yenu. Ama utalikubali, au . . . Sio kunikubali mimi, sio kukubali niliyosema, bali kuikubali Injili

yote, nguvu zote, Biblia yote, kila kitu ambacho Mungu anasema. Kikubali Hicho, la sivyo itakuwa imechelewa mno.

³⁷⁵ Sasa inueni tu mikono yenu na kuomba. Kama, nitawaacha muombe. Niliomba nikafaulu. Ninyi ombeni sasa. Ni juu yenu. Mungu awabariki. 

63-0126 Uwekezaji
Ramada Inn
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org